

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Saba – Tarehe 12 Septemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali. Swali letu la kwanza ni la Ofisi ya Rais – TAMISEMI, litaulizwa na Mheshimiwa Ibrahim Mohamedali Raza, Mbunge wa Kiembesamaki, kwa niaba Mheshimiwa Ali Khamis.

Na. 83

Kuwaondoa Omboomba – Dar es Salaam

MHE. KANALI MST. MASOUD ALI KHAMIS (K.n.y. MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI) aliuliza:-

Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na tatizo la omboomba wengi na katika baadhi ya maeneo wamejenga miundombinu ya kulala.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuwaondoa omboomba katika Jiji la Dar es Salaam?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Mohamedali Raza, Mbunge wa Kiembesamaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo ombaomba katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar-es-Salaam kwa sababu viro vivutio vingi ikiwemo watu wenye imani mbalimbali ambao huwapatia fedha na vitu vingine kama sehemu ya ibada. Kuzagaa kwa ombaomba kimekuwa chanzo kimojawapo cha uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na changamoto za ombaomba mara kadhaa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam imetekeleza hatua mbalimbali za kuwaondoa, ikiwemo kuwakamata na kuwasafirisha makwao, lakini wamekuwa wakirudi. Mfano mwezi Septemba, 2013 ombaomba 253 na watoto 135 walirejeshwa kwao ambapo watoto 33 walirejeshwa shulen. Hii inathibitisha kuwa wapo watu wazima wanaotumia watoto kuombaomba. Watanzania wanatakiwa kuzitumia fursa za kupambana na umaskini zilizoandaliwa na Serikali, ikiwemo elimu msingi bila malipo, huduma za afya vijijini na uwepo wa Sheria ya Fedha 2018 inayotoa fursa kwa makundi mbalimbali ya uzalishaji mali kupata mikopo, wakiwemo walemau. Vilevile watumie uwepo wa ardhi ya kutosha yenye rutuba kama fursa ya kuweza kujitegemea na hivyo, kujikomboa dhidi ya kuombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ombaomba wamekuwa wakisababisha watoto wengi kutopata fursa ya kusoma shule au kuwa watoro, nawaagiza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri chini ya usimamizi wa Wakuu wa Mikoa kuititia Kamati za Ulinzi na Usalama kuwakamata wototo wote ambao badala ya kwenda shulen huzagaa mitaani wakiombaomba, wakamatwe

pamoja na wazazi wao na washtakiwe Mahakamani chini ya Sheria ya Elimu ya mwaka 78 inayokataza utoro na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Kifungu cha 166, 167 na 169A vinavyohusu wajibu wa wazazi na walezi kwa watoto. Aidha, Mabaraza ya Madiwani nayo yanaweza kutunga Sheria Ndogo za kuzuia utoro pamoja na kudhibiti mienendo ya baadhi ya watu kuombaomba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kanali.

MHE. KANALI MST. MASOUD ALI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, tatizo la ombaomba lina muda mrefu na limekuwa likishughulikiwa na Serikali na likilizwa mara kwa mara lakini bado ombaomba wanaonekana wakirudi mitaani. Je, ni hatua gani madhuhuti sasa Serikali imeziweka ili hao ombaomba wasirudi tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kweli kama alivyosema Naibu Waziri, wakamatwe na washtakiwe, lakini je, hawa hawafanyi kwa makusudi, wanafanya kutokana na hali ngumu ya maisha. Je, wanapotoka huko gerezani baada ya kuwafunga na vitu vingine, hatua gani za Serikali zinachukuliwa kuwasaidia kimaisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, hatua ambazo Serikali inazichukua ni kutoa fursa kwa wananchi wote ili waweze kuzitumia kwa ajili ya kujikomboa kiuchumi na kupambana na umaskini. Hatua hizo nimezitaja kwenye jibu la msingi kama vile kutoa fursa mbalimbali za mikopo, kuwepo kwa ardhi ya kutosha yenye rutuba na vilevile kuwa na programu nyingi za kuboresha huduma mbalimbali katika

maeneo ya vijijini ili watu wasitoke vijijini wakaja mijini kufuata huduma hizo. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo ya hatua madhubuti lakini hii hatua ya kuwakamata na kuwarudisha makwao imeonekana ni kama vile haisaidii sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, hali ya maisha ni ngumu ni kweli na ndiyo maana nimesema kwamba tutumie hizo fursa. Kwa kusema ukweli fursa ya Elimu Msingi Bila Malipo ni muhimu sana tuifuatilie vizuri ili watoto wetu wote ambao wanastahili kuwa shulen i wawe shulen i.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombaomba wengi wamekuwa wanatumia watoto ambao wanatakiwa kuwa shulen i na wanazagaa hovyo mitaani, ndiyo maana nikatoa wito kwamba Sheria ile ya Elimu na Kanuni ya Adhabu itumike kikamilifu katika kuhakikisha kwanza watoto wote warudishwe shulen i na vilevile wazazi ambao hawatekelezi wajibu wao nao vilevile wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ngumu ya maisha, fursa ziko nyingi, naomba sana zitumike ili kujikomboa na hali ngumu ya maisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, amezungumza kwamba sababu nyingine inayochangia ni pamoja na imani za kidini na hali ngumu ya maisha. Ni kwa nini sasa Serikali isichukue jukumu la makusudi, kwa sababu tatizo la ombaomba kwa watu wengi ni *mindset*, la kuelimisha jamii kwa vipindi mbalimbali vyta redio na *television* kuhakikisha tunabadilisha mtazamo kusudi hawa watu kama ni imani za kidini waende kwenye imani wanazozi amini wakapate misaada huko badala ya kuwa barabarani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Jiandae Mheshimiwa Saada.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake ni mzuri na yeye ni kiongozi wa dini. Nadhani sababu mojawapo ya kuwepo kwa ombaomba wengi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba watu wengine wanatoa misaada kama sehemu ya ibada. Ndiyo maana unakuta ombaomba wengi siku kama za Ijumaa na Jumapili wanakuwa wengi zaidi katika maeneo hayo ambayo ni ya ibada ni kwa sababu watu wengine wanatoa fedha kama misaada. Kwa hiyo, kwa kweli kama ushauri wake ulivytotolewa tunauchukua kwa ajili ya kuupangia bajeti ya kutoa elimu kwa umma ili kusudi kupunguza hili tatizo la ombaomba.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Saada.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi fursa ambazo amezonesha ni pamoja na mikopo lakini tunajua kiukweli wale ombaomba hawana *asset* yoyote na taasisi zetu za kifedha mara nyingi zinahitaji *at least* uwe na *asset* au uwe na jambo linguine.

Sasa Serikali haioni umuhimu wa kupanga mkakati maalum *specifically* kwa ajili ya hawa ombaomba ili waondokane na hii hali waliyokuanayo *rather than* *generalise* wapate mikopo ambayo sio rahisi kiukwell?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba taasisi nyingi za kifedha zinadai *collateral* ili watu wapate mikopo, lakini kwenye utaratibu wetu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ambayo tumeipitisha mwaka huu hapa Bungeni ni kwamba, mtu atapata mkopo kutokana na shughuli anayofanya. Ndiyo maana nimetoa wito kwamba watumie fursa ya ardhi yenye rutuba kuzalisha mali.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hawa ombaomba watapata elimu nzuri kupitia halmashauri zao, Maafisa Maendeleo ya Jamii watoe elimu hiyo, wakajunga kwenye vikundi nya uzalishaji mali wanayo fursa ya kupata mikopo kupitia halmashauri, ile 10% ambapo 4% inakwenda kwa vijana 4% inaenda kwa wanawake na 2% inaenda kwa walemovu. Kwa hiyo, hiyo ni fursa mojawapo ambayo ni nzuri ya kupata mkopo bila kuwa na *collateral* au kuwa na *asset* yoyote. Jambo la muhimu sana ni Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii watumike kuelimisha wananchi ili watumie fursa zilizopo.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Gimbi Dotto, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Sware.

Na. 84

**Wamiliki wa Viwanda Wanaokiuka
Sheria ya Mazingira Nchini**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI (K.n.y. MHE. GIMBI
D. MASABA)** aliuliza:-

Tanzania inakabiliwa na tishio la mabadiliko ya tabianchi linalosababishwa na uchafuzi wa mazingira, hasa wa viwandani:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wamiliki wa viwanda wanaokiuka Sheria za Mazingira?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Doto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mhesimiwa Mwenyekiti, tatizo la mabadiliko ya tabianchi kwa kiwango kikubwa linasababishwa na uzalishaji wa gesi joto unaotokana na matumizi ya nishati kwa 47%, uzalishaji wa viwanda kwa 30% na usafirishaji 11% kwa shughuli za maendeleo katika nchi zinazoendelea kiviwanda hususan Ulaya, Marekani, Asia na Australia. Bara la Afrika kwa ujumla linachangia gesi joto kiasi kisichozidi 3%. Tanzania huzalisha kiasi cha tani 0.09 za hewa ukaa (*Per Capital Emission*) kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Tanzania inachangia kiasi kidogo sana katika tatizo la uzalishaji wa gesi joto ambazo ndiyo chanzo cha mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, pamoja na kuchangia kidogo kiasi hicho Tanzania imeendelea kuathirika kutokana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, kama vile kupungua kwa barafu ya Mlima Kilimanjaro, kuongezeka kwa usawa wa bahari, ukame, mafuriko ya mara kwa mara na mlipuko wa magonjwa. Tatizo kubwa linatokana na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na baadhi ya viwanda nchini kwa kutiririsha majitaka yenye sumu na kemikali ambazo huathiri sana viumbe hai pamoja na mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inayo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004. Sheria hii imeweka misingi ya usimamizi, tathmini na kuchukua tahadhari kuhusu madhara kwa mazingira, yakiwemo ya viwandani. Kwa kuzingatia sheria hii, Serikali imekuwa ikielimisha na kuwatoza faini wamiliki wa viwanda wanaokiuka sheria hii. Aidha, wamiliki wanaoendelea kukaidi maelekezo na masharti wanayopewa hufungiwa kufanya shughuli na hupewa masharti kabla ya kuruhusiwa kuendelea na shughuli zao tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa wito kwa wamiliki wa viwanda kuzingatia utekelezaji wa sheria na mikakati mbalimbali iliyopo kwa ajili ya kuwezesha usimamizi endelevu wa hifadhi ya mazingira kwa faida yetu na vizazi vijavyo. Wamiliki wa viwanda wanatakiwa kuhakikisha Tathmini ya AAthari kwa Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*) vinafanyika na kuzingatiwa. Aidha,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wamiliki wa viwanda wanapaswa kutumia nishati rafiki kwa mazingira na kutumia teknolojia banifu katika uzalishaji wa bidhaa zao ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, moja ya sababu inayosababisha mabadiliko ya tabianchi ni uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti. Kwa kuwa hapa nchini ukataji miti uko kwa juu sana kwa sababu watu wengi tunategemea nishati ya kuni au mkaa kwa ajili ya mapishi nyumbani na shughuli nyaginezo. Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba huu uharibifu wa mazingira kwa kutumia nishati hizi ambazo zinapunguza idadi ya miti nchini inakuwa imepunguzwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, majibu ya Serikali inaonesha kwamba wale wachafuzi wa mazingira kuptitia viwanda hutozwa faini au baadhi kufungiwa. Serikali haioni kwamba inafaa iwe na mikakati mahsusii ya kudhibiti viwanda hivi kuangalia miundombinu yake kabla haijanza kazi kwamba haitakuwa inaharibu mazingira?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwa nishati mbadala na sisi tumekuwa tukisisitiza na tumeanza mkakati huo na tumeshirikisha na ndugu zetu wa TFS sasa wanatoa miti ambayo inahimili ukame na wanatenga maeneo maalum kwa ajili ya kuvunwa na maeneo maalum kwa ajili ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia swali la pili namna ya kudhibiti wamiliki wa viwanda, kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu yangu ya swali la msingi kwamba tutaendelea kuzingatia sheria ileile. Niwaombe wamiliki wa viwanda wajue kabisa kwamba wanao wajibu wa kuyatunza mazingira na wanao wajibu wa ku-treat yale maji ambayo yanaleta zile taka hatarishi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, umejibu vizuri sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ruth Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Salim.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchafuzi wa viwanda, vileyile mifuko ya *plastick* ni source mbaya sana ambayo inachafua mazingira. Je, kwa nini Ofisi ya Makamu wa Rais haitumii ule Mfuko wa *Technological Transfer and Adaptation Fund* kuwawezesha hao wenye viwanda wabadilishe teknolojia waweze kuzalisha mifuko ambayo ni rafiki kwa mazingira?

MWENYEKITI: Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mifuko ya *plastick* imekuwa ikileta uchafuzi wa mazingira kwa kiasi kikubwa sana. Niseme tu kwamba, Serikali tayari ilishazuia kutoa leseni mpya kwa wazalishaji ama viwanda vipyta vinavyokuja kwa ajili ya mifuko ya *plastic*. Pia, tumeendelea ku-*encourage* wawekezaji wa viwanda vyta mifuko rafiki ili waweze kuwekeza na hatimaye huko mbele tuweze ku-*ban* kabisa mifuko ya *plastic*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake amesema kwamba wale wanaokiuka taratibu hizi sheria inawapa mamlaka ya kuwafungia ama kuwapiga faini, zote hizo ni *force approach*. Dunia ya leo ni dunia shirikishi, Wizara ina mpango gani wa kuwashirikisha na kuwaelimisha wenye viwanda na kushirikiana nao kuona tatizo hili linamalizwa kabisa badala ya kutumia nguvu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba kabla ya mwekezaji kuanza kuwekeza hatua ya kwanza sisi huwa tunatoa elimu. Mpaka afikie hatua ya kupata *certificate* ya *EIA*, maana yake amekidhi vigezo vyote. Kinachofuata akikiuka utaratibu ambao tumeuweka ni lazima tumpigie faini.

MWENYEKITI: Ahsante. Hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa Ignas Malocha.

Na. 85

Uharibifu wa Mazingira katika Ukanda wa Ziwa Rukwa

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Upo uharibifu mkubwa wa mazingira katika Ukanda wa Ziwa Rukwa unaotokana na ukataji miti ovyo, wingi wa mifugo na kilimo kisichozingatia utaalamu; shughuli hizi zinahatarisha kukauka kwa ziwa hilo kwa miaka ijayo:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti na wa haraka kunusuru ziwa hilo, hasa ikizingatiwa kuwa imegundulika gesi ya helium katika ziwa hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo Oktoba, 2016 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) alifanya ziara ya kutembelea Mkoa wa Rukwa na moja ya maeneo aliyotembelea ni Bonde la Ziwa Rukwa ambapo alitoa maelekezo ya kuanza mchakato wa kulitangaza Ziwa Rukwa kama eneo nyeti la mazingira kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutangaza eneo hilo kuwa eneo nyeti unaendelea na unatarajiwu kukamilika ifikapo mwishoni mwa kwa 2018. Eneo hilo litakapotangazwa rasmi kuwa eneo nyeti litakuwa chini ya usimamizi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mzingira (*NEMC*) ambalo kwa kushirikiana na wadau litaandaa mpango wa matumizi ya eneo husika hivyo kuongeza nguvu ya usimamizi wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri alielekeza Halmashauri zote ambazo zina eneo katika Bonde la Ziwa Rukwa kuweka alama za kuonesha mwisho wa umbali wa mita 60 kutoka kwenye kingo za Ziwa Rukwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na kuweka mabango ya kukataza shughuli zinazoharibu mazingira ndani ya umbali huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa eneo la Bonde la Ziwa Rukwa limebainika kuwepo kwa dalili ya gesi ya helium. Tathimini ya Athari ya Mazingira imefanyika katika hatua hii ya utafiti ili kuweza kubaini athari na madhara yoyote yanayoweza kutokea wakati wa zoezi hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa lakini vilevile nimpongeze kwa ufanuzi mzuri. Pamoja na ufanuzi, ninayo maswali mawili ya nyongeza. (*Makofii*)

Swali la kwanza, maeneo yenyе rasilimali muhimu kama hayo ya Ziwa Rukwa pamoja na maelekezo mazuri ya Serikali yanahitaji ufuatiliaji na usimamizi wa karibu. Je, toka Serikali imetoa maelekezo hayo umefanyika ufuatiliaji kujiridhisha kama mazingira hayo hayaharibiwi tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, rasilimali muhimu ya gesi ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia inaweza kuinua uchumi wa Tanzania na kukuza uchumi wa Taifa letu kwa ujumla. Je, Serikali ina mkakati gani kuanza kuchimba gesi hiyo ili Taifa linufalike kabla gesi hiyo haljaanza kuchimbwa mahala pengine duniani? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Malocha pia kwa ufuatiliaji wake mzuri na nimshukuru kwamba sasa kwenye eneo hili la Ziwa Rukwa tunaweza kuelekeza nguvu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linahusu ufuatiliaji. Kwa kweli tuna kila sababu ya kushirikiana naye kwa ajili ya kufuatilia hili kwa kushirikiana na wananchi na viongozi walioko kule. Mheshimiwa Malocha nadhani baada ya Bunge hili tutakuwa pamoja kwa ajili ya kwenda kufuatilia kuona yale maagizo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri yametekelezeka kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye eneo la gesi, ni kweli kabisa imegundulika gesi hii ya helium ambayo ni maalum kabisa katika nchi yetu na sisi kwenye eneo letu la mazingira tayari imeshafanyika Tathimini ya Athari ya

Mazingira kwa awamu ya kwanza kwa ajili *exploration*. Atakapopatikana mwekezaji kwa awamu ya pili tutakuwa tayari kuja kufanya tena Tathmini ya Athari ya Mazingira ili kuhakikisha kwamba gesi hiyo inapatikana na kuweza kutumika. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ziwa Tanganyika linamilikiwa na nchi nne: Burundi; Zambia; DRC Congo; na Tanzania. Hivi karibuni Ziwa Tanganyika upande wa Uvira DRC Congo ghafla limebadilika rangi na kuwa rangi ya kijani ingawa maji hayana rangi. Je, Wizara ya Muungano na Mazingira inayo taarifa hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mhusika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziwa hili linamilikiwa na nchi tatu na kuna Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority*) na juzi tulikuwa na mukutano hapa na viongozi wa Mamlaka hiyo kuzungumzia uhifadhi mzima wa Ziwa Tanganyika ikiwemo hili suala lakini pia suala kubwa zaidi la kukatika kwa ukingo kwenye Mto Lukuga ambao unatoa maji mengi kwenye Ziwa Tanganyika na kuyapeleka Mto Congo. Kwa hiyo, haya masuala mawili tunayaafutilia na tutampa mrejesho Mheshimiwa Mbunge kuhusu matokeo yake.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hamida Abdallah.

Na. 86

Mgogoro wa Ardhi – Mbuga ya Selous na Wananchi

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi kati ya Mbuga za Wanyama Selous – Kilwa na wananchi wanaoishi karibu na mbuga hiyo

umezidi kuwa mkubwa kwa sababu mipaka halali hajulikani. Kwa mfano, mwaka 1974 mpaka halali ulikuwa Mto Matandu, mwaka 2010 mpaka huo ulisogezwa kufikia Bwawa la Kihurumila katika Kijiji cha Kikulyungu:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuhakiki eneo hilo ili kuondoa mgogoro mkubwa uliopo kati ya Wanakijiji wa Kihurumila na Mbuga?

(b) Je, Serikali iko tayari kutatua mgogoro uliopo kati ya wananchi wa Kilwa na Mbuga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wa Pori la Akiba Selous uliwekwa kwa kuzingatia Tangazo la Serikali Na. 275 kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974. Tangu wakati huo hadi sasa mpaka huo haujafanyiwa marekebisho yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Kikulyungu na Pori la Akiba la Selous unatokana na kijiji hicho kutokukubaliana na uhakiki wa mpaka wa pori hilo uliofanyika mwaka 2010 kwenye eneo la Wilaya ya Liwale kwa kuwatumia wataalam kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu ilitembelea Pori la Akiba la Selous – Kanda ya Kusini Liwale tarehe 3 na 4 Agosti, 2018 na kukutana na wananchi na viongozi wengine wa Serikali ikiwemo Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa mgogoro huo. Kupitia ziara

hiyo, wananchi sasa wameridhia kazi ya uhakiki ifanyike upya na kuhakikisha kuwa watatoa ushirikiano kwa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; wanakijiji; na Halmashauri ya Mji kuhakiki mpaka wa Pori la Akiba Selous katika eneo la Kijiji cha Kikulyungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wananchi, wawekezaji na maeneo yaliyohifadhiwa, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wote katika uhakiki wa mipaka na uwekaji wa alama kwenye mapori yote nchini na kuandaa na kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamida.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri katika Bunge liliopita aliniahidi kuja Lindi kutembelea maeneo haya na kwa kweli alikuja na aliambatana na viongozi wa Mkoa na Wilaya katika kutembelea na kujionea maeneo haya ya mgogoro wa ardhi. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, mwaka 1974 mpaka huu ulikuwa Mto Matandu lakini mwaka 2010 katika marejeo ya mpaka, mpaka huu ulikuwa katika Bwawa la Kihurumila, Kijiji cha Kikulyungu. Napenda kujua ni kwa nini Serikali iliamua kuhamisha mpaka huu kutoka katika Mto Matandu na ukafika katika Bwawa hili la Kihurumila?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili napenda kujua sasa baada ya ziara yake na kujionea mwenyewe, nini sasa Serikali itafanya katika kumaliza mgogoro huu wa mipaka kati ya Serikali kuititia Selous na Serikali ya Wilaya ya Kilwa lakini na mpaka wa Wilaya ya Liwale na Selous?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote kwa maombi makubwa ambayo mmekuwa mkiyatoa kwa sababu siku ambapo tulikuwa tutatue hili tatizo ndiyo siku ambayo Mheshimiwa Waziri alipata ajali na hivyo ikalazimika kwamba tukatishe ile ziara na tuende kumhudumia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Mheshimiwa Waziri jana ametolewa hospitalini na sasa yupo nyumbani, kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa maombi yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kweli kwa muda mrefu amekuwa akilifuatilia tatizo hili na sisi kama Serikali ndiyo maana tuliamua kwamba hilli tatizo sasa lifike mahali lifikie mwisho. Naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, si kweli kwamba Serikali ilisogeza mpaka ilitokana tu na tafsiri. Tafsiri ya mpaka iliyandikwa kwenye GN ya mwaka 1974 ndiyo wataalam walipotafsiri wakaona mpaka unapita wapi. Hata hivyo mwaka 2010 wananchi hawakuridhika ndiyo maana tukaamua kwamba kwa sasa hivi tufanye tena upya kwa kutumia wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjulische Mheshimiwa Mbunge kwamba kutokana na hiyo ziara na maagizo ambayo tulikuwa tumeshayatoa tumeamua kwamba Kamati rasmi kutoka Wizara ya Ardhi iko tayari inapitia mpaka wa Ruangwa na Kilwa ili kurekebisha ile mipaka na baada ya hapo tarehe 18 Septemba wataenda katika Kijiji cha Kikulyungu ambapo wataangalia mpaka wa Kijiji cha Kikulyungu pamoja na mpaka wa Selous. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba baada ya hapo tatizo hili litakuwa limekwisha kwa sababu wananchi wameahidi kushirikiana vizuri kabisa na hiyo Kamati. Naomba tu ushirikiano na Mheshimiwa Mbunge awe na subira.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gashaza na Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi. Niipongeze Serikali kwanza kwa kazi nzuri iliyofanyika kwenye mapori ya hifadhi ya wanyamapori Kimisi, Burigi na Bihamramlo kwa kuondoa mifugo na sasa hifadhi hizo zimepanda hadhi kuwa *National Parks*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna tatizo hususani kwa Maafisa ya Wanyamapori ambao siyo waaminifu ambao sasa wanaenda vijiji na kuswaga mifugo kuingiza kwenye pori la hifadhi kwa lengo la kutengeneza mazingira ya rushwa. Serikali inachukua hatua gani kwa maafisa hawa ambao sio waamini? Hili limetokea Ngara na ushahidi upo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, hatua za rushwa.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Gashaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza na ni kweli kabisa kwamba Serikali imepandisha mapori matano katika eneo lile kuwa sasa ni Hifadhi ya Taifa. Naomba nitumie nafasi hii kumjulisha tu kwamba baada ya kupandisha hayo mapori sasa hakuna shughuli yoyote ya kibinadamu au uwindaji wowote unaoruhusiwa katika maeneo hayo kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi za Taifa. Kwa hiyo naomba tu tuendelee kushirikiana na kuhakikisha kwamba hayo hayatokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba wafanyakazi wetu wanakamata mifugo na kuiingiza kwenye hifadhi halafu ndiyo wanaomba rushwa, naomba nitumie fursa hii kusema kwamba kwanza wafanyakazi hawaruhusiwi

kufanya hivyo na pale ambapo inabainika wafanyakazi wetu wanakiuka maadili ya kiutumishi basi tunaomba taarifa wananchi watusaidie kututajia kwamba kuna mfanyakazi huyu na huyu anaomba rushwa nasi tutachukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, katika maeneo yote ya mapori nchini hairuhuswi mifugo wala kilimo kuingia katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwaombeni hakuna mwananchi yeoyote anayeruhuswi kuingiza mifugo ikiingizwa itataifishwa na hivyo ndio sheria inavyoelekeza. Kwa hiyo, naomba ushirikiano na wananchi wote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kuna mgogoro unataka kufukuta katika Jimbo langu kwenye Kata ya Nyatwali inayojumuisha wakazi zaidi ya 11,000. Lile sio Pori la Akiba ni maeneo yao ambayo wanaishi, inasemekana Serikali inataka kuwashamisha hajjawashirikisha, hawajui wanaenda wapi na wanalipwa nini. Nini tamko la Serikali kuondoa hili tatizo kwa sababu mna migogoro mingi msitengeneze migogoro mingine na Bunda hatutakubali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza kwa jinsi ambavyo anawateea wananchi wake. Niseme tu kwamba mpaka sasa hivi hatuna taarifa rasmi kwamba tunataka kuihamisha hiyo Kata ya Nyatwali. Kwa hiyo, kama kuna fununu za namna hiyo lazima zitazingatia taratibu na sheria zote zilizopo kuhakikisha kwamba wananchi wanashirikisha kikamilifu na viongozi wote wanashirikisha ndipo hapo wananchi wanaweza kuhamishwa. Kama

wananchi watakuwa waliingia kinyume na taratibu hapo ndiyo lazima nguvu zitatumika lakini kama siyo hivyo nikuhakikishie tu kwamba wananchi watashirikishwa vizuri kabisa ili kuhakikisha kwamba sheria inazingatiwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chegeni na Mheshimiwa Chumi.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa vile sasa kuna mgogoro mwingine umeanza kuzuka kati ya wananchi na wanyama waharibifu kama tembo na viboko. Je, Serikali inasaidiaje wananchi ambao wanaishi kando kando ya hifadhi hizi pamoja na ziwa kuepukana na mgogoro huu ambapo sasa tembo wanajeruhi watu na kuharibu mali za watu pamoja na kuuwa watu lakini viboko wanafanya uharibifu mkubwa sana wa mazao ya wananchi. Serikali ina mpango gani sasa kuwasaidia wananchi hawa kuondokana na mgogoro huu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na changamoto ya wanyama wakali na waharibifu katika maeneo mengi nchini lakini Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba inawaelimisha wananchi ipasavyo kuhakikisha kwamba wanakabiliana na hao wanyamapori pamoja na kuweka maafisa katika kila wilaya kuhakikisha kwamba wanashirikiana na wananchi na wale wa vijiji kuhakikisha kwamba wanawadhibiti hao wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kutumia Kikosi chetu cha Kupambana na Ujangili (KDU) na katika maeneo yale ambayo imeoneka kwamba wanyama wale wamezidi

tumekuwa tukichukua hatua za kufungua kituo katika hilo eneo ili kuhakikisha askari wetu wanakuwepo hapo kwa muda mrefu na ili kuwadhibiti hao wanyama wakali na waharibifu. Kwa hiyo, naomba tu tuendelee kushirikiana tuhakikishe kwamba tunapambana na hao wanyama wakali na waharibifu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Wakati katika baadhi ya maeneo kumekuwa na migogoro baina ya Serikali na hayo maeneo ya mbuga za wanyama, lakini kuna maeneo mengi ya utalii kwa mfano maeneo ya kihistoria kama kule Iringa Isimila kuna maeneo yana maporomoko ya maji ambayo pia ni kivutio cha utalii na kuna maeneo yana misitu na ndege wazuri ambapo ni vivutio vya utalii. Je, Serikali haloni sasa ni wakati muafaka wa kuwekeza nguvu kutangaza vivutio hivyo ili walao kupunguza *pressure* huko kwenye mbuga za wanyama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nchi yetu imebahatika kuwa na maeneo mengi ya vivutio vya utalii ikiwemo misitu, malikale, maeneo ya historia na mambo mengine. Hivi sasa Serikali imetengeneza mkakati mkubwa wa kuhakikisha kwamba vivutio vyote vinatangazwa ipasavyo ili kuhakikisha utalii wa ndani na utalii wa nje unaongezeka katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumechukua hatua kuhakikisha kwamba Mikoa ya Kusini tunapanua utalii ili kupunguza *pressure* kubwa upande wa Kaskazini. Tunaamini jitihada hizi zitazaa matunda makubwa na kuhakikisha kwamba vivutio vyote vinafahamika na watalii wengi wanaongezeka zaidi nchini.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo na swali la Mheshimiwa Felister Bura.

Na. 87

Kuanzisha Mfuko wa Uendelezaji wa Zao la Alizeti

MHE. FELISTER A. BURA aliuliza:-

Wananchi wa Kanda ya Kati ni wakulima wazuri wa zao la alizeti:-

Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko kuanzisha Mfuko mahsus wa uendelezaji wa zao la alizeti?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nalbu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na jitihada mahsus za kuendeleza zao la alizeti ambazo ni pamoja na kuwa na Mfuko wa Kuendeleza zao hilo. Kutokana na umuhimu huo, Serikali kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Mkakati wa Kuendeleza zao la Alizeti nchini (*Sunflower Development Strategy 2016 – 2020*) ambapo unalenga kuongeza uzalishaji na tija; kuboresha ubora wa mbegu za alizeti; kuimarisha tasnia ya alizeti kwa kuboresha uratibu miongoni mwa wadau; kuchochea ukuaji wa tasnia ya alizeti kwa kuweka sera wezeshi; na kuhakikisha uwepo wa masoko ya uhakika kwa mazao ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa ili kufanya biashara na pia kushirikiana na wadau wengine katika kuendeleza mazao

mchanganyiko. Hivyo, Bodi hiyo haiwezi kuanzisha Mfuko wa kuendeleza zao la alizeti peke yake bali kwa kushirikiana na wadau wengine wa zao la alizeti. Aidha, pale itakapokubalika, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko itakuwa ni mionganoni mwa wadau muhimu wa kuanzisha Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo wadau wa alizeti wamekuwa wakikutana kujadili changamoto mbalimbali ya zao hilo na kuzitafutia ufumbuzi. Katika kurasimisha jitihada hizo na kuwa na Jukwaa la Wadau, Wizara ilitisha kikao cha wadau kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuendeleza zao la alizeti hususan katika upatikanaji wa mbegu bora, huduma za ugani na teknolojia bora za usindikaji wa alizeti. Aidha, katika ushirikishwaji huo wa wadau, suala la Mfuko wa Kuendeleza zao la Alizeti Ilitajadiliwa kwa kina na kama inaonekana ni muda muafaka wa kuanzisha Mfuko huo, wadau watakulaliana kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uanzishwaji wa mifuko zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara tayari zipo jitihada za kuimarisha utafiti wa mazao ya mbegu za mafuta ambapo kwa zao la alizeti Taasisi ya Utafiti wa Kilimo TARI imejipanga kuendeleza kusafisha mbegu za awali aina ya “Record” kwa ajili ya kuzalisha madaraja ya msingi na hatimaye daraja la kuthibitishwa. Kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za alizeti kupitia Wakala wa Mbegu wa Taifa (*Agricultural Seed Agency-ASA*) na kuhamasisha makampuni binafsi ya kuzalisha mbegu bora za alizeti.

Aidha, katika jitihada hizo, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Muungano wa Wazalishaji wa Zao la Alizeti Tanzania (*Tanzania Sunflower Processors Association – TASUPA*) na Mfuko wa Kuendeleza Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Market Development Trust-AMDT*) katika kuhakikisha wakulima wa alizeti wanapata mbegu bora na huduma za kilimo bora cha alizeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Naibu Waziri kwa kuteuliwa lakini pia nimpongeze kwa majibu mazuri aliyonipatia. Pamoja na majibu hayo mazuri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Taifa hili hutumia fedha nyangi sana kuagiza mafuta ya kula ukiachilia mafuta ya petroli, lakini nchi hii ina uwezo wa kuzalisha mafuta ya kutosha ya kula na tukaacha kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi. Katika nchi yetu kuna viwanda vingi vinavyokamua mafuta kwa mfano, Kiwanda cha *Mount Meru* ambacho kina uwezo wa kukamua mafuta tani 400,000 lakini kwa sasa wanapata tani 40,000 tu ukiachilia viwanda vingine.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha kwamba Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara wanawekwa kwenye mkakati maalum wa kuzalisha mazao ya mafuta na hata Mkoa wa Kigoma unaozalisha mafuta ya mawese, kwamba sasa mkakati uwekwe kwa kupata mbegu bora kwa ajili ya kuzalisha mazao yanayozalisha mafuta, ni mkakati gani umewekwa na Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sisi wananchi wa Dodoma ni wakulima wazuri sana wa zabibu na tunazalisha mara mbili kwa mwaka lakini hatuna soko. Zabibu zinaoza mashambani kwa sababu wakulima wamekosa masoko. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba zabibu zote zinazozalishwa na wakulima zinapata soko? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kutaka kujua mkakati wa Serikali kwa ajili ya kuweza kuzalisha mazao ya mbegu ya mafuta hapa nchini ili kumaliza tatizo la mafuta hapa nchini ili kuokoa fedha za kigeni. Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 4 Juni, 2018 ilizindua Programu Maalum ya Kuendeleza Kilimo, kwa Kiluguru tunaita *ASDP* // ambapo lengo lake ni kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mpango huo Mheshimiwa Waziri Mkuu alianza utekelezaji huo tukaenda Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya kuzindua na kuendeleza kilimo cha mchikichi, ikafuatiwa na kikao cha wadau kilichofanyika tarehe 24/05 pale Morogoro kwa maana ya kampuni yetu ya uzalishaji mbegu ya *ASA*, Kampuni ya Utafiti wa Mbegu (*TARI*) pamoja na Kampuni ya Udhibiti wa Mbegu (*TOSCI*) wamepanga mikakati na tumekubaliana kama Serikali kuanza kufufua zao la mchikichi kwa ajili ya kuzalisha ndani ya miaka minne miche milioni 20 ili kumaliza tatizo hilo sambamba na kuongeza mbegu bora katika zao la alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu zabibu, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwatetea watu wake wa Dodoma ambao ni maarufu kwa kilimo cha zabibu hapa nchini lakini ni kweli bei ya *wine* inayotokana na zabibu ya Tanzania ipo juu kuliko ya wine zinazotoka nje ya nchi. Hii inatokana na sababu ya gharama kubwa za uzalishaji hapa nchini na tija ndogo wanayopata wakulima, wanatumia gharama kubwa lakini wanapata faida ndogo. Serikali tumeliona hilo na kwa sasa tunapitia na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuangalia mfumo wa kodi zetu na ushuru ili kupunguza gharama za uzalishaji kuweshesha *wine* hii kuuzwa kwa bei nafuu ili soko liwe la uhakika. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante umejibu vizuri sana. Mheshimiwa Leah jiandae Mheshimiwa Aisharose.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mazingira ya Mkoa wa Simiyu yanafanana na

mazingira ya Mikoa ya Kati kwa zao la alizeti lakini wakulima wa Simiyu wamekuwa wakilima zao hili kwa kubahatisha mbegu za alizeti zisizo na tija ukililinganisha na Mikoa ya Kati. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuleta mbegu zenyetija ikiwemo na kutoa elimu kwa wakulima wa Mkoa wa Simiyu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa majibu yangu ya swalii la msingi nilizungumzia mikakati iliyopo kwa Shirika letu la ASA, *TOSKI/na TARI*. Mbegu zipo na nawaelekeza watu wa ASA wapeleke mbegu kule kwa Mheshimiwa Mbunge ili mbegu hizi zipatikane kwa gharama nafuu kwa hii mbegu aina ya *Record*. Pia kuna makampuni binafsi ambayo yamethibitishwa na Taasisi yetu ya Kudhibiti Ubora ya *TOSCI* yanauzua mbegu kihalali nayo nayaomba yapeleke mbegu katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge ili wananchi wapate mbegu kwa urahisi zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Aisharose, jiandae Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. AIASHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Singida ni wakulima wazuri wa zao la alizeti, je, Serikali haionti umefika wakati sasa wa kulifanya zao hili la alizeti kuwa ni zao la kimkakati ili kuongeza tija na kipato kwa wananchi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la alizeti ni moja ya zao la kimkakati. Kama unavyofahamu kipaumbele cha kwanza cha Serikali ni mazao ya chakula na alizeti ni moja ya mazao

ya chakula. Kwa hiyo, lipo kwenye zao la kimkakati na ndiyo maana lipo chini ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wanasyansi wamefanya utafiti na wanasema kwamba vyombo vya plastiki vikikutana na joto kali vinasababisha madhara makubwa sana kwa afya ya binadamu kwa sababu yanatoa kemikali fulani inayoitwa BPA. Je, Serikali inalitambua hili na kama inalitambua inachukua hatua gani kuwasaidia wakulima hawa wa alizeti ambao wanaauza mafuta yao barabarani na yanapigwa juu kali sana? Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanahifadhi mafuta hayo ipasavyo ili wananchi wetu wasipate madhara hasa ya kansa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bidhaa za plastiki kuwekea vyakula hasa vya moto kuna madhara yake lakini kwa haya ya baridi bado tunafanya utafiti katika Serikali na tumeshaagiza taasisi zetu za utafiti wafanye utafiti kujua madhara yanayopatikana kwa mafuta kuwekwa kwenye vyombo vya plastiki ili wakituletea majibu tutakuja kumpa Mheshimiwa Mbunge.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango na swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji.

Na. 88

Vigezo Vinavyoainisha Ukuaji wa Uchumi Nchini

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitangaza kukua kwa hali ya uchumi wa nchi yetu kila mwaka:-

Je, ni vigezo gani sahihi vinavyoainisha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa, vigezo sahihi vinavyoainisha ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote duniani ni ongezeko la pato la Taifa, ongezeko la pato la wastani la mwananchi kwa mwaka, ongezeko la uuzaaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi, kupungua kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, utulivu wa bei za bidhaa na huduma, utulivu wa viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni na kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo na huduma za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji unaofanywa katika nchi ni kigezo kingine cha msingi cha ukuaji wa uchumi kwa kuwa huongeza kasi ya uzalishaji wa bidhaa na huduma, ajira, kipato cha mwananchi mmoja mmoja, pato la Taifa na hatimaye kupunguza umaskini katika jamii. Aidha, mchango wa Serikali katika ukuaji wa uchumi ni pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuwekeza zaidi kwenye shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi, kupunguza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi na kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa na huduma nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize kwa makini

swali langu likukune mithili ya nazi na unipe jibu mfano wa tui. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, nakubaliana na maelezo uliyoyatoa juu ya uanishaji wa kukua kwa uchumi wa nchi. Mheshimiwa Waziri lakini katika kipindi hiki ambacho tunashuhudia pato la Taifa likiwa limesimama la dola 976 mpaka mwaka 2016, tunashuhudia upungufu wa uuzaaji wa bidhaa nje ya nchi, tunashuhudia bei za huduma zikitetereka mfano majengo ambapo sasa hivi yanakosa wapangaji, tunashuhudia fedha yetu ikiendelea kushuka... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali lako.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna uhusiano gani wowote ambaao unaonesha kweli hali ya uchumi inakua wakati hali ya wananchi kukosa pesa inazidi kuongezeka mionganoni mwetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nchi za kiafrika zimeingia katika mtego au mahusiano na China inayosababisha wote kukimbilia kukopa China. Jambo hili linasababisha wanaposhindwa kurejesha mikopo kukamatiwa mali zao na tayari baadhi ya nchi jirani zimeanza kukamatiwa mali zao na kudhibitiwa na China. Je, mnachukua tahadhari gani kwa nchi yetu kuja kutumbukia katika mfumo huo wa kuja kukamatiwa nchi yetu na ikawa koloni la China? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatib Said Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimwambie pato la Taifa halijasimama wala halijashuka. Tumeendelea kuleta taarifa sahihi ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu ukuaji wa uchumi wa Taifa letu, tumeonyesha jinsi

gani unakua na nimeonyesha vigezo hivi na kitakwimu Mheshimiwa Khatib tuwasiliiane ili nikupatie takwimu ujue taifa letu linakwenda wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza amezungumzia wananchi kukosa pesa, naomba nimwambie Mheshimiwa Khatib na Bunge lako Tukufu kwamba *money supply* kwenye uchumi siyo kigezo cha kukua kwa uchumi wa Taifa. *Money supply* kwenye uchumi inaonesha kwamba Taifa hilo limeshindwa ku-control ukuaji wa uchumi wake. *In short run* inaweza ukajidanganya ukuaji wa uchumi upo lakini *in long run* matatizo na madhara yake ni makubwa sana. Nimpongeze sana Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania pamoja na wataalam wake wanafanya kazi kubwa kuhakikisha hakuna pesa za ziada kwenye uchumi wetu ili tusiingie kwenye matatizo makubwa ya kiuchumi, hilo ni jibu la kwanza kwa swali la Mheshimiwa Khatib. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lako la pili, hizi ni *speculative* ambazo zipo kwenye vyombo vyta habari. Napenda kumwambia kwamba kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tupo makini sana wapi tunakwenda kukopa, kwa riba ya kiasi gani na kwa nini tunakwenda kukopa. Ndiyo maana sasa hivi Bunge lako Tukufu linajadili Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma, ni umakini ule ule wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano kuhakikisha Taifa letu linakwenda kuwa salama. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri bado anaona kwamba uchumi unakua wakati masoko ya wananchi ya mazao yao hayapo, hakuna *annual increment* kwa wafanyakazi, hakuna mazingira mazuri ya wafanyakabiashara wetu kufanya biashara jambo ambalo limesababisha *stress* kwa wananchi na tumeshuhudia matukio

ya watoto kuchomwa moto kwa upotevu wa Sh.2,000 na mwanafunzi kuuawa kwa sababu ya Sh.75,000...

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Kwa nini bado anaona uchumi unakua wakati *stress* hizi zimesababisha matukio makubwa katika Taifa letu? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naamini uchumi wa Taifa unakua ni kwa sababu ya takwimu na hali halisi ya uchumi wetu ulivyo.

Napenda kuliambia Bunge lako tukufu na uniruhusu nisome kipengele hiki kwenye mkutano uliokwisha mwezi uliopita wa Wakuu wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (*SADC*) yalisemwa haya yafuatayo kuhusu uchumi wa Taifa letu, naomba kusoma, mkutano uliombwa *ku-note that the majority of member states underperformed in achieving the agreed microeconomic indicators only three member states of SADC have attained that and all these three countries is Botswana, Lesotho and Tanzania.* (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Taifa letu unakua, watu wa nje wanaona kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Watanzania wanayaona na tupo imara tutaendelea kusimamia uchumi wa Taifa letu. (*Makofî*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na swali la Mheshimiwa Ester Bulaya.

Kilimo cha Umwagiliaji katika Mji wa Bunda

MHE. ESTER A. BULAYA aliuliza:-

Kilimo cha umwagiliaji katika Mji wa Bunda kimekuwa kikitengewa fedha kidogo sana kiasi cha kutokidhi mahitaji kazi husika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Ofisi ya Umwagiliaji ya Wilaya ili kufanya kilimo kuwa cha kisasa, endelevu na chenye kuleta tija kwa wananchi wa Bunda?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ester Amosi Bulaya, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya miradi ya umwagiliaji ili kuboresha kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP I*), Serikali ilijenga mabwawa mawili ya Maliwanda na Kisagwa na kujenga skimu tatu za umwagiliaji zenyeki hekta 220,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa skimu katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Bunda. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuendelea kuboresha kilimo cha umwagiliaji ili kiweze kuleta tija na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na malighafi kwa ajili ya viwanda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Waziri katika majibu yake wataalam wanajibu kana kwamba bado Halmashauri ni moja lakini tuna Halmashauri mbili; Halmashauri ya Wilaya ina majimbo mawili ya Mwibara kwa Mheshimiwa Kangi na Bunda kwa Mheshimiwa Boniphace; Halmashauri ya Mji ina Jimbo moja tu la Ester Bulaya, Bunda Mjini. Sasa haya majibu walijompa ni ya enzi zile za babu, za Wasira, sio kipindi hiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester, uliza swali.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza maswali yangu mawili ya nyongeza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara kwenye Jimbo langu la Bunda alitembelea Kikundi cha Igebesabo kilichopo Kata ya Nyatwali ambacho kina mradi mkubwa wa umwagiliaji uliogharimu zaidi ya shilingi milioni 700. Pale wana changamoto ya mashine kubwa ya kusukuma maji ambayo yanatoka Ziwa Viktoria aliwaahidi atawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini ahadi hii itatekelezwa kwa sababu pia katika hicho kikundi kuna vijana kama wewe Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Idara ya Umwagiliaji ina changamoto nyingi ikiwepo ya bajeti na vitu vingine, lakini kwa sasa hivi hawana gari la kuweza kufanya *patrol* katika miradi mbalimbali ya umwagiliaji katika Wilaya nzima ya Bunda. Ni lini sasa watawapatiwa gari ili sasa kilimo cha umwagiliaji Bunda kiweze kushamiri na vijana wengi *graduates* sasa hivi wamejajiri wenye kwenye shughuli za umwagiliaji?

MWENYEKITI: Ahsante, umeshaeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa maswali mazuri lakini kubwa ambalo nataka nimhakikishie, ahadi ni deni. Kwa kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha tunaitimiza kwa wakati ili wananchi wake, kwa maana ya kile kikundi, waweze kupata mashine hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala zima la gari, ili mradi uwe bora na wenye tija kwa wananchi lazima kuwe na usimamizi na ufuatiliaji wa karibu. Kwa hiyo suala la gari ni jambo la muhimu sana. Niagize wataalam wetu wa Bunda kufuatilia kitendea kazi hiki na sisi kama Wizara ya Maji tutatoa ushirikiano wa dhati kabisa katika kuhakikisha kinapatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kitandula, Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Qambalo.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Mwakijembe ambayo imetumia fedha nyngi kujengwa, zaidi ya shilingi bilioni moja, mpaka leo hii haijakamilika kwa kukosa mifereji ya umwagiliaji lakini vilevile kukosa bwawa na sasa tunashuhudia maeneo ya wananchi yakichukuliwa na Jeshi bila fidia yoyote. Je, Waziri yuko tayari kuja kufanya ziara mahsusil Jimboni Mkinga ajionee hali hii ili kuweza kutatua tatizo linaloikabili skimu ile?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, ni ziara tu, kama uko tayari muambie. Jiandae Mheshimiwa Shikilindi na Mheshimiwa Qambalo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kaka yangu, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, mimi kama Naibu Waziri wa Maji nipo tayari.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shikilindi na Mheshimiwa Qambalo.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakulima wa mbogamboga wa Wilaya ya Lushoto wanachimba vidimbwi vidogovidogo kwa ajili tu ya kunyeshea mazao yao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kwa kuwajengea mifereji hasa wakulima wa mabondeni hasa Mabonde ya Boheloi, Mshizii, Kwai, Milungui, Ubiri, Kwekanga, Mazumbai, Mlola, Mboi hadi Makanya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu, Mheshimiwa Shekilindi (Bosnia), kwa kazi nzuri anazozifanya katika Jimbo lake la Lushoto. Kubwa ambacho nataka nimwambie ni kwamba nchi yetu sasa hivi tunakwenda katika uchumi wa kati, tumeona haja sasa ya kulima kilimo cha umwagiliaji. Nimhakikishie kwamba sisi Wizara yetu ya Maji tumetenga shilingi bilioni 29.767 katika kuhakikisha tunawekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Niwaombe tu wataalam wetu wa Lushoto wasilale, wamsaidie Mheshimiwa Mbunge katika kuhakikisha jambo lake linatimilika kwa wakati.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Qambalo.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya Mawaziri wa Wizara hii kutembelea chanzo cha maji cha Mto Qangedded kule Karatu ambacho kinatumiwa na wananchi katika kilimo cha umwagiliaji zaidi ya vijiji sita. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari sasa kutimiza ahadi yake ya kutembelea eneo hilo ili kutatua changamoto ambazo wakulima wa eneo hilo wanakumbana nazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilihakikishie Bunge lako nilliahidi kwenda kutembelea Jimbo la Karatu lakini kutokana na changamoto sikuweza kufanikisha ahadi ile. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kabla ya Bunge la Novemba tutatimiza ahadi ile kwa kuhakikisha tunatembelea miradi katika jimbo lake.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

Na. 90

Ahadi ya Ujenzi wa Daraja la Mto Wami

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE aliuliza:-

Ni Sera ya Serikali kuhakikisha mawasiliano baina ya watu wake katika maeneo ya nchi yanawezeshwa na kujengwa kikamilifu:-

Je, Serikali imejipangaje kuhusu utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa Daraja la Wami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa Daraja la sasa la Wami lenye urefu wa mita 88.75 liliopo Mkoa wa Pwani ambalo ni jembamba ni kiungo muhimu katika Barabara Kuu ya Chalinze – Segera. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imeanza maandalizi ya ujenzi wa daraja jipya litakalojulikana kwa jina la Daraja Jipya la Wami (*New Wami Bridge*) ambapo mnamo tarehe 28 Juni, 2018, ilisaini mkataba wa ujenzi na Kampuni ya *Power Construction Corporation* ya Nchini China kwa gharama ya Sh. 67,779,453,717 na muda wa ujenzi ni miezi 24. Daraja Jipya la Wami litakuwa na urefu wa mita 513.5 na upana wa mita 11.85 na litajengwa umbali wa mita 670 pembedi ya daraja la zamani kwa upande wa chini yaani Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu na wananchi kuwa ujenzi wa daraja hili jipya utagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 na utajumuisha ujenzi wa barabara unganishi za daraja kwa pande zote mbili zenye jumla ya kilometra 3.82 ili kuweza kuunganisha daraja jipya na Barabara Kuu ya Chalinze – Segera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mkandarasi yuko kwenye hatua ya maandalizi ya ujenzi, yaani ujenzi wa ofisi na nyumba za wafanyakazi pamoja na kuleta vifaa, mitambo na wataalam ili kazi ya ujenzi wa daraja ianze.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka nimkumbushe tu kwamba jambo hili lipo ndani ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Ilani na kwa kuwa ni msikivu na Mheshimiwa *Eng. Kamwelwe* ni msikivu zaidi, naomba jambo hili walismamie ili liweze kukamilisha ndoto ya Watanzania ambao wamekuwa wanalala pale, hasa panapotokea matatizo ya ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii dogo, pamoja na matatizo yaliyopo katika Daraja la Wami, lakini pia iko ahadi ya Serikali ya kutengeneza barabara inayotoka Mbwewe - Mziha - Kibindu, je, hili jambo nalo Mheshimiwa Waziri mmeefikia wapi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nizipokee pongezi nyingi ambazo amezitoa kwa Serikali, lakini pia nimpongeze yeye binafsi kwa namna anavyofuatilia masuala mbalimbali katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ya Mbwewe – Mziha – Kibindu inafanyiwa matengenezo makubwa. Kuhusu kuiboresha barabara hii, nimuombe tu Mheshimiwa Ridhiwani, kwa sababu ni mfuatilaji mzuri, baadaye tuonane ili tuangalie kwenye bajeti na mipango yetu ili niweze kumpa taarifa sahihi ili aweze pia kuzitumia kuwalishaa wananchi wa Jimbo la Chalinze. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swalii nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Itoni – Manda kuanzia eneo la Nundu kuititia Kata za Uwemba, Luponde na Matola, ni barabara ambayo imeahidiwa miaka mingi sana na Serikali kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Nataka kufahamu, ni lini hasa kazi hii itaanza kutekelezwa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mhusika, majibu. Jiandae Mheshimiwa Dkt. Kawambwa na Mheshimiwa Mbarouk.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kuhusiana na Barabara ya Itoni – Manda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile tayari tumeshaanza kuitekeleza na ndiyo barabara pekee ambayo inajengwa kwa kiwango cha zege kilometra 50 kutoka Lisitu - Mawengi. Tumeanza na hilo eneo tukaacha kilometra 50 ambazo zinaingia kwenye jimbo lake, lakini nimhakikishie kwamba na hizo 50 nazo tuko kwenye hatua ya kukamilisha taratibu tuweze kuzitangaza ili iweze kuunga sasa kutoka kwenye lami kwenda barabara ya zege.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa na Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali imetenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bagamoyo - Pangani - Tanga. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kama yuko tayari ujenzi huo kutumia wakandarasi wawili ili mmoja aanze Tanga mwagine aanze Bagamoyo kwa madhumuni ya kuharakisha ujenzi lakini kuwapa faraja pia wananchi wa pande hizo mbili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Mbarouk.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anatambua kabisa hatua nzuri za ujenzi wa barabara hii upande wa Serikali tulipofikia kwa vile anaendelea kufuatilia vizuri. Nichukue tu wazo lake kama ushauri ili wakati sasa wa kuanza ujenzi tutaona namna nzuri ya kufanya *lotili* tuone kama hilo analolisema tunaweza tukalifanya tutaweza kulitekeleza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nishukuru kwa kilio chetu watu wa Kanda ya Kaskazini...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu siyo rafiki. Mheshimiwa Mbarouk, endelea.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa sisi watu wa Kanda ya Kaskazini kwa maana ya Mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimajaro, Manyara na Pwani, kilio chetu kusikilizwa na Serikali kwa ujenzi wa Daraja Jipyaa la Wami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na ujenzi wa daraja jipyaa, tatizo kubwa limekuwa ni magari aina ya *semi* kushindwa kupanda milima sababu ya mlima mkali uliopo pale. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweka magari maalum ya kusaidia kuvuta haya magari ya *semi* pale ambapo yanashindwa kupanda milima kama ilivyo kwa njia ya Kasumulu *Boarder* karibu na Malawi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbarouk, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magari kushindwa kupanda katika milima ni suala ambalo kwa upande wa Serikali tunaendelea kulitazama kwa sababu ya ukuaji wa teknolojia na magari yanayokuja sasa yamekuwa ya kisasa zaidi. Tunaliangalia kwa upana wake kwa sababu kwa *records* za ajali ambazo zimetokea hivi karibuni tunayo pia mashaka ya kuona namna gani magari haya yanakuja ya kisasa lakini pia madereva ambao wanaendesha magari haya waweze kupata elimu ili waweze kumudu kuyaendesha. Kwa hiyo, mara nyingi unaona *technical faults* zinazotokea inawezekana kuwa uko uwiano kati ya teknolojia mpya na elimu ambayo wanaipata madereva wetu. Kwa hiyo, tutaendelea kulifuatilia ili tuweze kutatua tatizo hili.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kidogo.

Wageni kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika; wageni saba wa Mheshimiwa Spika ambao ni Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Ufaransa: *Senator Ronan Dantec, Chairperson of Parliamentarians Friends of Tanzania and Leader of the Delegation; Honorable Frederic Clavier, French Ambassador to Tanzania; Senator Cyril Pelleah, Member of Parliament; Senator Bernard Jomier, Member of Parliament; Charlotte Montigny, Protocol Officer; Mona Mahecha, Official from MOFAEC and Mariam Kilongo, official from MOFAEC. Welcome to the Parliament of Tanzania and you can now please proceed to your meeting. Thank you very much. (Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mtuka.

Kampuni ya Simu ya Viettel Kutekeleza Mkataba

MHE. DANIEL E. MTUKA aliuliza:-

Kampuni ya Simu ya Viettel (Halotel) imepewa zabuni ya kusimika minara ya mtandao wa simu katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Kasi ya usimikaji wa minara hiyo ni ndogo; mfano Vijiji vya Hika – Sanza hakina mawasiliano ya simu kabisa:-

Je, Serikali ina mkakati gani thabiti wa kuibana kampuni hiyo ili kutekeleza mkataba wake kwa wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya Mtandao ya Viettel kuhusu utekelezaji wa mpango wa mawasiliano. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 16 Julai, 2014 ukiwa na mpango wa kukamilisha utekelezaji wake ndani ya miaka mitatu hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2017. Katika mkataba huo makubaliano ya kufikisha mtandao wa mawasiliano ya simu kwenye vijiji 4,000 yalitakiwa kufanyaika katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ni kufikisha mtandao wa mawasiliano ya simu kwenye vijiji 1,800 ifikapo Novemba, 2015; awamu ya pili ni kufikisha mtandao wa mawasiliano ya simu kwenye vijiji 1,200 kwa kipindi cha Novemba, 2015 hadi Novemba, 2016 na awamu ya tatu kufikisha mtandao wa mawasiliano ya simu kwenye vijiji 1,000 kwa kipindi cha Novemba, 2016 hadi Novemba 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Julai, 2018, jumla ya vijiji 3,712 vilikuwa vimefikiwa na mtandao wa mawasiliano ya simu. Aidha, ucheleweshwaji na utekelezaji wa mradi huu umechangiwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upatikanaji wa vibali vya ujenzi wa minara hususani kwenye maeneo ya hifadhi za Serikali, mbuga za wanyama na kadhalika ambapo vibali vimekuwa havipatikani kwa wakati. Vilevile taratibu za masuala ya mazingira zinazoratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) zinachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali kuitia ukaguzi wa mradi na vikao mbalimbali inaendelea kusimamia utekelezaji wa mkataba wa Kampuni ya Simu ya Viettel ili kuhakikisha kwamba makubaliano yaliyowekwa yanakamilishwa. Aidha, usimikaji wa minara kwa ajili ya mtandao wa simu katika Vijiji vya Hika, Igwamadete, Isimbanguru, Mangoli na Mafulungu unatarajiwaka kukamilika mwishoni mwa Septemba, 2018. Hivyo, baada ya kukamilika kwa minara itakayosimikwa katika maeneo hayo kipande cha barabara ya Manyoni – Hika – Sanza kitakuwa na mawasiliano ya simu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtuka.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pamoja na majibu hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, utetezi wa mkandarasi kwamba kulikuwa na changamoto za kupata vibali vya ujenzi kwa kweli haina mashiko kabisa kwa sababu mimi kama Mbunge na Mkurugenzi wangu tulishirikiana na mkandarasi huyu vibali vikapatikana kwa muda mwafaka na akajenga minara miwili ikakamilika pamoja na kujenga msingi wa mnara mmoja wa tatu. Ni muda wa mwaka mmoja na nusu sasa minara hiyo haijawashwa. Ni lini atakamilisha kazi hii kwa sababu tunahitaji mawasiliano Manyoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, utoaji wa huduma za mawasiliano umeligawa jimbo langu, kwa mfano, Kata ya Makulu na hasa Kijiji cha Hika hakina mawasiliano kabisa hata upande juu ya mti huwezi kuwasiliana na watu na unakuwa umeshajitenga na dunia kabisa.

Je, ni lini Serikali italeta huduma hii ya mawasiliano katika kata hii, hasa katika Kijiji cha Hika? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazo taarifa za kuchelewa kuwashwa kwa minara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja katika eneo hili la Sanza na Sasilo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mwishoni mwa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi unaokuja hii minara hii itawashwa. Kwa hiyo nakuhakikisha Mheshimiwa na nikupongeze sana kwa kufuatilia juu ya suala hili na niwahakikishie wananchi kwamba sasa watapata mawasiliano muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, niseme tu kwamba eneo hili la Makulu Mheshimiwa Mbunge amelitaja kwamba tunayo orodha ya vijiji vingi ambavyo tayari viko kwenye hatua sasa ya kuweka minara tunavyo vijiji 369 orodha ninayo hapa Mheshimiwa Mbunge. Lakini pia tunakamilisha hatua za manunuzi mwanzoni mwa mwezi ujao tutakuwa na orodha nyingine mpya ya vijiji vingi tu ambavyo tutaenda kujenga minara.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha maeneo ambayo yana shida ya minara na mawasiliano hafifu tunaendelea kuyaboresha ili wananchi Watanzania kwa ujumla waweze kupata mawasiliano ambayo ni muhimu katika harakati za maendeleo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mipata atafuatiwa na Mheshimiwa Nachuma.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi.

Katika Bunge liliopita niliweza kuorodhesha vijiji vya kata tatu ambavyo havina mawasiliano mazuri Kata ya Kala vijiji vyote; Kata ya Sintari kijiji kimoja na Kata ya Ninde vijiji viwili, nataka kujua, Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha kwamba mawasiliano yanapatikana katika vijiji hivyo? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema katika jibu langu la msingi ni nayo orodha ya vijiji vingi hapa. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuwasiliane ili tuweze kuona hivi vijiji katika hizi Kata tatu alizozijata pamoja na hii Kata ya Kala na Minde ili tuweze kuona kwa sababu tunaendelea kupeleka hii huduma ya minara. Kwa hiyo, nakuomba tu tuwasiliane ili uwe na uhakikika kwamba vijiji vyako na kata hizi zote ziko katika hiyo orodha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nachuma.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kumekuwa na ahadi nyingi sana na za muda mrefu kwenye mitaa ya pembezoni mwa Manispaa ya Mtwara Mikindani ambayo hakuna mawasiliano maeneo hayo na nimekuwa nikichangia ndani ya Bunge hili na kuyataja maeneo hayo kwa muda mrefu kwamba maeneo ya Namayanga, maeneo ya Naulongo, Mkunjanguo, Mbawala Chini na Mkangara, mawasiliano hayapo kabisa ya simu. Je, ni nlini Serikali hii itapeleka mawasiliano kwenye mitaa hii ambayo ni muhimu ndani ya Manispaa ya Mtwara Mikindani? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mahitaji ni mengi ni kweli ahadi ni nyingi, lakini ni ukweli pia kwamba ahadi nyingi tunaendelea kuzitekeleza kadri tunavyokwenda.

Nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla, kadri tunavyoweka minara katika maeneo mbalimbali na baada ya minara kuwashwa bado tunahitaji kuona changamoto ambazo zitakuwa zimejitokeza baada ya hii minara kuwashwa kwa sababu suala la mawasiliano ni suala ambalo baada ya kuwashwa minara inaweza ikajitokeza baadhi ya maeneo yakawa na uhafifu wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaomba tu tuendelee kuwasiliana pamoja tunavyoendelea kutekeleza ahadi hizi. Lakini pia tuendelee kupata *feedback* baada ya minara kuwashwa ili tuhakikishe kwamba maeneo yote yanafikiwa na mawasiliano haya kuititia minara yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Wilaya ya Kakonko takribani kata sita zimepakana na nchi ya Burundi na Kata ya Lugenge na Kasuga nazo pia zimepakana na maeneo hayo ambayo hayana mawasiliano kwa njia ya simu. Mawasiliano ni hafifu na ni shida kabisa, nataka kujua, ni lini Serikali itapeleka minara katika maeneo hayo kiusalama kwa sababu maeneo hayo yamekaribiana na nchi ya Burundi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi nikupongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kuna mambo mengi kweli unafuatilia katika maeneo haya. Ni kweli maeneo haya yaliyo mpakani yana usumbufu mkubwa hii ni pamoja na mwingiliano kwa sababu niwahi

kutembelea maeneo haya utaona kabisa kwamba tunapata mawasiliano kutoka nchi za jirani. Tutahakikisha tu Mheshimiwa Mbunge tunajenga minara ili pia iweze kupunguza ule mwingiliano wa mawasiliano ambayo yanatokea nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe pia tuwasiliane nina orodha ndefu hapa ili tuje tuone maeneo haya kama hatujaya-*cover* basi tuendelee kupeleka minara mingine.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani*.

Na. 92

Ujenzi wa Reli ya Kusini

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Reli ya Kusini (*Southern Circuit*) ya Mtwara - Mbambabay - Mchuchuma - Liganga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wetu umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali napenda kufanya rekebisho dogo ni kwamba isomeke ni Mbunge wa Tunduru Kaskazini, siyo Tunduma. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imedhamiria kujenga reli ya Kusini kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga baada ya upembuzi yakini fu uliofanywa mwaka 2016 na Kampuni ya KORAIL ya

Korea kuonesha kuwa mradi huu unaweza kurejesha gharama za uwekezaji za sekta binafsi kutokana na fursa lizizopo katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa umbembuzi yakinifu huo Mhandisi Mshauri alipendekeza mradi huu utekelezwe kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi na umma yaani *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) imetenga kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kumpata mshauri wa uwekezaji yaani *Transaction Advisor* wa kuandaa andiko la kunadi mradi huu na kutafuta wawezekaji kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi na sekta ya umma (*PPP*), tathimini ya kumpata *Transaction Advisor* mahili inaendelea baada ya kujitokeza washauri 12 wanaoshindanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa andiko Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) litatangaza zabuni katika vyombo mbalimbali vya habari kwa lengo la kumpata mwekezaji mahiri na mwenye masharti yanayovutia. Aidha, naomba ushirikiano wa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kupata wawekezaji mahili katika endelezaji wa reli hii muhimu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makani.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napongeza majibu mazuri ya Serikali. Lakini la pili nampongeza pia huyu Mhandisi Mshauri Kampuni ya KORAIL kwa kuona kile ambacho hata kufanya upembuzi yakinifu wa wakitaalamu sana kinaonekana.

Kwa kuwa tunazungumzia mradi ambao unakwenda kuhudumia au kutafuta au kutumia fursa za kiuchumi zinazotokana na madini chuma, lakini pia makaa ya mawe, lakini mazao ya kilimo lakini pia urani lakini pia fursa za Ziwa Nyasa zinazotokana na shughuli za uvuvi kutaja machache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na majibu haya mazuri ya Serikali mwaka 2016 mpaka leo ni takribani miaka mitatu tangu upembuzi yanikifu ukamilishe kazi yake utoe matokeo.

Sasa je, Serikali inajipangaje kuharakisha utekelezaji wa mradi huu katika hatua inayofuata? Swalii la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali naamini kwamba amesema mimi kama muuliza swalii mmojawapo wa Wabunge na wenzangu wengine Bunge zima tuweze kushirikiana na Serikali kwa kutekeleza jukumu letu la kuisimamia na kuishauri Serikali; na mimi nilikusududia hapo mwanzo kabisa kwamba niweze kuijandaa kwa hoja binafsi kuhusiana na mradi huu. Lakini kwa wakati huu na kwa sasa hivi na majibu haya ya Serikali ya leo yakiniridhisha basi nitaondoa ile azma yangu ya kwenda kwenye hoja binafsi.

Je, inawezekana kuunda Kamati Ndogo ya Wabunge ili waweze kushirikiana kwa karibu kabisa na Serikali katika kutafuta huyo *Transaction Advisor*? Ama hata hao wawekezaji ili tuweze kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge nikuambie kwamba Liganga na Mchuchuma zimekuwepo, mali hii ni ya nchi na kwamba sasa wakati muafaka umefika kwamba sasa mali hii lazima itumike kwa ajili ya manufaa ya nchi. Tayari kama ulivyosema tangu mwaka 2016 Serikali iliona kwamba wakati muafaka umefika, tunahitaji kutumia haya madini kutookana na mahitaji ya kunyanya uchumi wa nchi. Taratibu zimeshafanyika, *Transaction Advisor* sasa hivi anatafutwa ili kwenda kwenye mwelekeo sasa ya kupata mwekezaji ambaye ni mzuri atayekubalika na taratibu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwamba shughuli hii inafanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu, ushauri wako ni mzuri Mheshimiwa Mbunge. Lakini sioni kwamba sasa hivi kwa vile mambo yanaendelea kwamba Bunge. Kwa hiyo, niombe tu kwamba uiachie Serikali kwa sababu imeshaanza.

MWENYEKITI: Ahsante.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, na inakwenda vizuri.

MWENYEKITI: Umeshaeleweka, Waheshimiwa muda wetu si rafiki kabisa muda wa maswali umekwisha na bado tuna maswali, tuendelee Wizara ya Elimu Mheshimiwa Paschal Haonga.

Na. 93

**Makato Makubwa kwa Wanufaika wa Mikopo ya
Elimu ya Juu**

MHE. PASCAL Y. HAONGA aliuliza:-

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeongeza makato kwa wanufaika wa mikopo kutoka asilimia 8 hadi 15 bila kuwashirikisha wadau mbalimbali pamoja na wanufaika wa mikopo.

(a) Je, Serikali haioni kwamba imevunja mkataba wa makubaliano kwa kuwa wakopaji walisaini mkataba wa asilimia 8 na siyo asilimia 15?

(b) Ongezeko la makato limewaathiri sana wakopaji na kuwafanya kuwa omibaomba na kuishi maisha magumu sana. Je, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haioni kama litakuwa jambo la busara kusitisha makato hayo ya 15% mara moja ili kunusuru maisha ya watumishi waliokopa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Paschal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijavunja mkataba wowote na wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu. Kilichofanyika mwaka 2016 katika marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo Sura ya 178 ni kuiboresha sheria hiyo kwa kutaja kiwango mahususi cha asilimia 15 kinachopaswa kukatwa kutoka mshahara ghafi wa wanufaika. Kabla ya marekebisho hayo kifungu cha 7(1)(h) kiliipa Serikali mamlaka ya kupanga kiwango cha makato na kubadilisha kiwango pale itakapoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuku hakikishia kuwa Serikali inafahamu umuhimu wa kuwashirikisha wadau katika marekebisho ya sheria yoyote, hivyo basi, katika mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 ya mwaka 2016 wadau mbalimbali walishirikishwa na wadau hao ni pamoja na wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi *TUGHE* na *TUCTA*, Chama cha Mawakili nchini (*MLS*) pamoja na wanafunzi kutoka Taasisi za Elimu ya Juu kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma pamoja na Chuo cha Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makato ya asilimia 15 kutoka kwenye mshahara ghafi wa wanufaika wa mikopo yamewekwa kisheria kwa lengo la kuhakikisha fedha zinazotolewa na Serikali zinarejeshwa kwa wakati ili ziweze kuwasomesha Watanzania wengine ambao wanauhitaji. Hivyo kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kusitisha makato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wanufaika wote wa mikopo ya elimu ya juu nchini kuhakikisha kwamba wanarejesha mikopo yao kwa wakati kwani wapo Watanzania wengi ambao

wanahitaji mikopo hiyo ili iweze kuwanufaisha wahitaji wengine. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano tangu iingie madarakani haijawahi kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma, lakini Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambacho ni chombo cha Serikali kimeongeza makato kutoka asilimia nane hadi asilimia 15. (*Makof*)

Je, Serikali iko tayari sasa kusitisha nyongeza hiyo ya makato hadi pale ambapo itaongeza mshahara kwa Watumishi wa Umma? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa ongezeko la makato kutoka asilimia nane hadi 15 limewaathiri sana watumishi wa umma maudhurio kazini kwa kukosa nauli.

Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka sasa kusitisha makato haya ya kutoka asilimia nane hadi 15 kwa kuwa watumishi wengi sasa hawana nauli na suala hili limeweza kuathiri maudhurio watumishi kazini na kupunguza ufanisi wa kazi? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza katika majibu yangu ya msingi Serikali haina mpango wowote wa kusitisha makato ya asilimia 15 ya wanufaika wa mikopo. Naomba kwamba watu wasichanganye mambo kwa sababu unapokata asilimia ya mshahara italipwa kulingana na kiwango chako cha mshahara wewe kama unapata shilingi 100,000 asilimia 15 itakuwa ni ya 15,000 na anayepata milioni moja atalipa 150,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, makato haya yanazingatia uwiano na ukubwa wa mishahara, lakini Serikali haitasitisha kama ambavo nimesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwaasa na kuwaonya watumishi ambao wanataka kusingizia makato ya asilimia 15 kwa kuchelewa kazini Serikali itachukua hatua za kinidhamu. Kwa sababu watumishi wote wa umma wanapaswa kuzingatia sheria kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wa umma.

WABUNGE FULANI: Sio sawa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea muda wetu siyo rafiki, Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 94

Hasara Iliyotokana na Vitabu Vyenye Dosari

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilikusanya vitabu vyenye dosari viliviyosambazwa shule za msingi nchini.

(a) Je, Serikali imepata hasara kiasi gani kutokana na dosari hiyo?

(b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa waliosababisha hasara hizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imeondoa vitabu ambavyo vilikuwa shulenii ambavyo vilisambazwa mwaka 2017 ambavyo vilibainika kuwa vina makosa. Katika utekelezaji wa hatua hiyo Serikali ilizingatia taarifa ya tathimini iliyo fanyika kuhusu vitabu hivyo na taarifa hiyo iliainisha vitabu vilivyokuwa na makosa ya kimaudhui na vile ambavyo havikuwa na makosa ya kimaudhui. Vitabu ambavyo vimeondolewa shulenii ni vile ambavyo vina makosa ya kimaudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania limeagiza Menejimenti ya Taasisi kuitia vitabu vyote vilivyoondolewa shulenii na kufanya tathimini ya ukubwa wa makosa ili hatimaye kukokotoa hasara iliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania iliwasimamisha kazi watumishi 29 ili kupisha uchunguzi wa chanzo cha dosari mbalimbali za vitabu. Uchunguzi huu umefikia hatua ya watumishi hao kuandikiwa mashitaka ya kinidhamu ambapo yakithibitika hatua stahiki zitachukuliwa kwa majibu wa sheria.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza hapo hapo awali tulikuwa na chombo ambacho kilikuwa kinapitia hivi vitabu na vifaa vyaa elimu *EMACK* kabla ya kwenda mashulenii. Na kwa kuwa *EMAC* ilifutwa rasmi, sasa niulize Serikali ina mpango gani wa kuanzisha chombo kingine au chombo mbadala ambacho kitakagua vitabu na vifaa vyaa elimu kabla ya kwenda mashulenii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni dhahiri kwamba sasa hivi kuna upungufu mkubwa sana wa vitabu

kwa shule za msingi hasa darasa la kwanza mpaka la tatu; je, Serikali ina mpango gani wa haraka ili kutatua changamoto hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli Serikali ilivunja *EMAC* ambayo ni *Education Management Approve Committee* iliyokuwa inahusika na kuitisha machapisho na vitabu vya elimu baada ya chombo hicho kushindwa kutekeleza wajibu wake vizuri na tulishuhudia kwamba pamoja na kuwepo kwa chombo hicho, lakini bado vitabu vilikuwa na makosa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba sasa hivi kazi ya kupitisha vitabu inafanywa na Taasisi ya Elimu Tanzania, lakini niseme kwamba Serikali itaangalia namna ya kuangalia utaratibu mwingine, baada ya kuondoa *EMAC* kwa sababu pia Taasisi ya Elimu inakuwa inaelemewa na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa vitabu, naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba sasa vitabu vimekwishafanyiwa marekebisho na zaidi ya nakala 9,000 za vitabu vya kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu vimekwishasambazwa shulenii, kwa hiyo, sasa hivi tatizo hilo Serikali imekwishesambaza vitabu vilivyorekebishwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Sayansi na Teknolijia, Dkt. Steven Lemomo Kiruswa. Waheshimiwa Naomba radhi muda wetu ni mdogo sana

Na. 95

Elimu ya Shule za Awali

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha elimu ya awali?

(b) Kwa kuwa msingi mzuri wa elimu huanzia katika shule za awali. Je, Serikali haioni kuwa ni jambo la muhimu kuanzisha shule za awali na kuajiri walimu waliofuzu kutoa elimu hiyo katika shule za vitongoji hasa vijijiini tofauti na ilivyo sasa ambapo jamii ndiyo inayozianzisha na kuziendesha shule hizo kwa kutumia walimu wasio na taaluma?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa elimu ya awali kabla ya mtoto kuanza darasa la kwanza na kwa kutambua umuhimu huo Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuboresha elimu hiyo ikiwemo kutenga vyuo 18 ambavyo vinatoa mafunzo kwa ajili ya kuandaa walimu wa elimu ya awali ili kuongeza idadi ya walimu wa kufundisha wanafunzi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inaboresha mtaala na muhtasari wa elimu ya awali na kutoa mafunzo kwa walimu kwa ajili ya utekelezaji wa mtaala huo na kuandaa vitabu vya kiada vya aina sita pamoja na vitabu vya ziada 12 vya hadithi kwa ajili ya elimu ya awali ambavyo tayari vimekwishaandaliwa na sasa viko katika hatua ya uchapaji. Pia Serikali imehakikisha kuwa kila shule ya msingi inakuwa na darasa la elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za elimu zinazelekeza watoto wa elimu ya awali wanapaswa kufundishwa na walimu waliosomea elimu ya awali au kupata mafunzo kazini kuhusu ufundishaji wa elimu ya awali. Hivyo Serikali itaendelea kuimarisha mafunzo ya ualimu wa elimu ya awali sambamba na kuendelea kuimarisha madarasa ya elimu ya awali.

MWENYEKITI: Dkt. Lemomo.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Waziri hususan anaponieleza mkakati wa Serikali katika kuinua kwango cha elimu ya awali. Namshukuru sana kwamba ametamka wazi kwamba kuna vitabu vya kiada vinachapishwa na kuna vitabu vya ziada viko katika mchakato wa kutolewa. Sasa swali langu la kwanza ni kwamba, je, vitabu hivi vitasambazwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa inaonekana Serikali imejikita kipeleka madarasa ya elimu ya awali katika shule za msingi kwa kuzingatia kwamba jamii nyingi za kifugaji wanaishi katika Wilaya kwa mfano Wilaya yangu ya Longido, Simanjiro, Kiteto, Ngorongoro na Monduli hata Siha wanaishi mbali na shule kutokana na jiografia. Sasa Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba elimu hii bora katika ngazi ya awali inawafikia watoto hawa wadogo ambaao hawawezi kufikia hizo shule zenyе madarasa ya awali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana muda wetu umekwisha.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusiana na vitabu katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tayari vitabu sita vya kiada; na vitabu vya kiada ni vile ambavyo ni lazima kwa mujibu wa muhtasari mwanafunzi awenavyo tayari vimekwishachapwa ambavyo viko katika hatua ya uchapaji ni vitabu vya ziada yaani vya nyongeza zaidi ya vile ambavyo ni vya lazima katika muhtasari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake la pili kuhusiana na umbali wa shule, kama nilivyosema Serikali imetoa maelekezo kwamba kila shule ya msingi ni laizma iwe na darasa la awali. Kwa hiyo, nitoe wito kwake nafahamu kwenye jamii za wafugaji kunakuwa na changamoto kwamba Hal mashauri ishirikiane na Serikali Kuu kuona kwamba kama kuna utaratibu wa tofauti na uliowekwa na Serikali wa kuchukuliwa kwa ajili ya jamii za wafugaji Serikali

iko tayari. Lakini Halmashauri ndiyo ina jukumu la kutoa mapendekezo pale ambapo wanaona utaratibu wa kisera ni mgumu kulingana na mazingira yao.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Uvubi, Mheshimiwa Koka.

Na. 96

Uboreshaji wa Mazao Yatokanayo na Mifugo

MHE. SILYVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha bidhaa za nyama nchini pamoja na mazao mengine yatokanayo na mifugo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ulishasimama ukakaa tena.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugona Uvubi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatekeleza mpango mkakati wa kuendeleza sekta ya mifugo ambaa unelanga katika kupunguza umasikini na kuboresha mazingira rafiki na endelevu katika uzalishaji wa mifugo yenye tija kwa kuzalisha mitamba milioni moja kwa mwaka kutokana na makundi ya ng'ombe wa asili kwa kufanya uhimilishaji, kuimarisha upatikanaji wa uhakika wa maji, malisho na vyakula bora vyia mifugo, kuhamasha matumizi ya teknolijia za ufugaji wa kisasa, kuboresha afya, masoko, biashara na uongezaji wa thamani wa mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara inatekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo na matumizi ya

dawa, chanjo na viwatilifu vya mifugo nchini ambapo inatarajiwa kupunguza vifo vya mifugo kwa zaidi ya asilimia 80 pamoja na kuwa na mifugo bora kwa ajili ya masoko ya ndani na nje kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mkakati huu unatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo; kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya mifugo kutoka asilimia 2.8 hadi asilimia 5.2; kuongezeka kwa mchango wa sekta ya mifugo katika pato la Taifa kutoka asilimia 6.9 hadi asilimia 9; kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo kama vile kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa 789,000 ambaa tulionao hii leo hadi kufikia ng'ombe wa maziwa milioni tatu; kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 2.4 hadi kufikia lita bilioni 3.8 kwa mwaka; kuongeza uzalishaji wa nyama kutoka tani 679,992 hadi tani 882,100; kuongeza uzalishaji wa ngozi kutoka futi za mraba milioni 89 hadi kufikia futi za mraba milioni 98.9 na kuongeza uzalishaji wa mayai bilioni 3.2 hadi bilioni 6.4. Pia mkakati unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa huduma za ugani, kuongeza uzalishaji wa chanjo za mifugo zinazozalishwa hapa nchini, kupongeza usindikaji wa mazao na mifugo pamoja na kuongeza usambazaji wa teknolojia za ufugaji bora ili kufikia wafugaji wengi zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Koka.

MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nia njema ya Serikali kurejesha baadhi ya maeneo ya shamba la mitamba la Kibaha kwa wananchi, kuna eneo dogo ambalo wananchi wanalikalia linaitwa maarufu Vingunguti. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari mimi na yeye kwenda kukutana na wananchi ili kuona muafaka kati yao na shamba hili la mitamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa machinjio ya kisasa yaliyokuwa yanajengwa pale kwenye Ranchi ya Ruvu ina zaidi ya miaka minne haijaendelea na

ujenzi na huku mahitaji ya nyama bora ni makubwa kwa Pwani na Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi wa machinjio haya hata kwa ubia katika wananchi na Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza anataka kujua kama niko tayari kwenda Kibaha na nataka kumhakikishia niko tayari kwenda Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, anataka kujua nini msimamo wa Serikali juu ya machinjio ya kisasa ya pale Ruvu. Ni kweli mradi huu umekawia, lakini kuititia mradi wa uendelezaji wa sekta ya kilimo, Serikali ya Korea imeonesha nia ya kutukopesha dola za Kimarekani takribani millioni 50 ambapo hivi sasa utaratibu Serikalini unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na moja ya miradi ambayo itakwenda kunufaika na pesa hizi ni pamoja na machinjio ya kisasa ya Ruvu ambayo haitaishia kaktiak kuwa machinjio tu, tutakuwa na *Leather Complex* ambayo itakwenda kutengeneza na uchakataji wa ngozi. Pia vilevile tutakuwa tayari kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi kuititia mradi huu wa machinjio ya pale Ruvu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri. Wizara ya Ardhi Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

Na.97

Kurahisisha Upatikanaji wa Vitabu vya Usajili wa Ardhi

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi walio kwenye vijiji viliviyopo kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuwarahisishia upatikanaji wa vitabu vya usajili Wilayani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA YA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba tano ya mwaka 1999 kifungu la 21 na Kanuni ya 36, kila kijiji chenye mpango wa matumizi bora kwa ardhi inapaswa kuwa na daftari la usajili wa ardhi ambalo linatunzwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji. Daftari la usajili ni daftari ambalo hutumika kusajili hati za hakimiliki za kimila zinazotolewa katika ardhi ya kijiji husika. Utoaji wa hatimiliki za kimila hutanguliwa na zoezi la uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ambayo inalenga kuboresha mipango ya matumizi ya ardhi katika kijiji kwa kuondoa mgongano wa matumizi katika ardhi za vijiji pamoja na kuiongezea thamani ardhi hiyo kuifanya kuwa ni mtaji hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwepo na changamoto za upatikanaji wa madaftari ya usajili wa ardhi katika baadhi ya Halmashauri kutokana na uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuchapisha madaftari hayo. Katika kutatua changamoto hiyo, Wizara imekuwa ikisadiana na Halmashauri kuzipatia madaftari ya usajili wa ardhi wakati wa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hata hivyo, Wizara imeanza kutoa hati za hakimiliki za kimila kwa kutumia mfumo wa kielektroniki katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga, Malinyi, Mkoani Morogoro. Teknolijia hii itakapoenea katika maeneo yote nchini itaondoa kabisa mahitaji ya madaftari ya usajili wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahimiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuchapisha madaftari ya usajili wa ardhi wakati

tunasubiri teknolojia ya utaji wa Hatimiliki za kimila kwa njia ya kielektroniki kuenea katika nchi nzima.

MWENYEKITI: Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, hata hivyo nina maswali mafupi.

Swali la kwanza; katika baadhi ya Wilaya, Vijiji pamoja na Kata mpango huu wa kupima ardhi mpaka kupata hatimiliki unachukua muda mrefu kiasi wananchi wanaumbuka, wanahangaika wakifutilia hati zao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hawa kusudi waweze kutumia muda mfupi wasitumie muda mrefu na Hatimiliki zao ziweze kupatikana kwa muda mfupi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; napongeza Serikali kwa kuanza kupima ardhi kwenye Mkoa wa Morogoro katika Wilaya za Ulanga, Kilombero pamoja na Mvomero; na huu mpango wa kupima ardhi unapunguza migogoro ya ardhi kwa upande wa wafugaji pamoja na wakulima.

Je, nauliza Serikali, mpango huu utakamilika lini kwa kupima ardhi kwenye Mkoa wote wa Morogoro kwenye Wilaya zake saba ambazo itasaidia kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekithiri kwa muda mrefu katika Mkoa huu wa Morogoro? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA YA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la kwanza amesema kwamba mpango wa matumizi bora ya ardhi unachukua muda mrefu na hatimaye watu wanachelewa kupata hati zao. Napenda tu nilifahamishe Bunge lako, mpango wa matumizi bora ya ardhi hauwezi kwenda kwa kasi kama tunavyotarajia kwa sababu inategemea pia maridhiano kati ya wanakijiji na matumizi yao katika maeneo yale ambapo unapoandaa mpango huo lazima uhusishe

makundi yote ya wafugaji, wavuvi na kila watu walioko pale na lazima pia waangalie ukubwa wa ardhi yao walijonayo na mpango wanaotaka kuweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima uende taratibu kuhakikisha kila mmoja ameshirikishwa na amekubaliana na mpango, sasa hatuwezi kwenda kwa kasi kwa sababu unashirikisha. Pengine labda elimu iendelee kutolewa hata kabla hatujafika sisi basi elimu iendelee kutolewa ili watu waone umuhimu wa kupanga mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao ili kuепusha migogoro ambayo mara nydingi inajitokeza.

Swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anaulizia ni lini tutakamilisha kupima ardhi yote katika Mkoa wa Morogoro na kuondoa migogoro iliyopo. Napenda nimhakikishie tu kwamba mpango wa Wizara tulionao siyo wa Morogoro tu, Morogoro ilikuwa ni eneo la mfano katika zile Wilaya tatu ambazo zilikuwa na migogoro pia ili kuweza kujua gharama za upimaji tukitaka kupanua mpango huu utatugharimu kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naona kwamba zoezi lile pale limekwenda taratibu sana kwa sababu linahusisha Wananchi na pia kuweza kujua tunawezaje kukamilisha kupima katika nchi nzima. Ni mpango wa Wizara kuhakikisha kila kipande kinapimwa sasa usoefu wa Morogoro utatusaidia *ku-scale up* upimaji na kuweza kujua gharama halisi zinazoweza kutumika na mpango huu tunaendelea nao na kwenye bajeti pia tumeonesha hivyo naomba tu Waheshimiwa Wabunge wawe na subira wakati Wizara inajipanga vizuri.

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 13 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mbunge), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni viongozi kutoka *Skype International*, waandaaji wa *Miss Journalism World 2018*.

Mashindano haya yatafanyika Jijini Arusha mwishoni mwa mwaka huu wakiongozwa na Ndugu Philemon Mollel, karibuni. (*Makof!*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Juma Aweso, Naibu Waziri wa Maji ambaao ni viongozi kutoka Jimbo la Pangani Mkoani Tanga wakiongozwa na Ndugu Rajabu Abdulrahman. (*Makof!*)

Wageni 19 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaao ni wasaidizi wa Sheria kutoka Wilaya saba za Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Ndugu Augustino Ernest. (*Makof!*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Victor Mwambaliaswa ambaao ni Wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Sangambi kutoka Chunya Mkoani Mbeya. (*Makof!*)

Wageni 48 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini na Mheshimiwa Mussa Ntimizi ambaao ni walimu watatu na wanafunzi 45 kutoka shule ya sekondari ya Jitegemee iliyopo Jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Ntimizi nao walisoma shule ya sekondari ya Jitegemee, karibuni. (*Makof!*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ni Mchungaji Ashery Magomba na Mama Mchungaji Helena Elenel kutoka Mpwapwa Mkoani Dodoma.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Maftaha Nachuma ambaao ni watoto wake kutoka Mkoani Mtwara, Ndugu Faudhia Maftaha na Ndugu Dinna Abdu Sungura. Kuna wageni 41 wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambaao ni jirani zake kutoka Nzuguni, Jijini Dodoma. (*Makof!*)

Mgeni wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Mabaharia kutoka Jiji la Dar es salaam, Ndugu Mohamed Momboka. Wageni wawili wa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambaao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Grace Kapinga na Ndugu Rehema Nakanje. Pia kuna

wageni 10 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni viongozi wa Chama cha Wasioona Tanzania wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Ndugu Robert Bundala. (*Makofi*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 120 na walimu 11 kutoka shule ya Jumapili ya Kanisa la Moravian-Tanzania Jimbo la Kaskazini Jijini Dodoma. Pia kuna wageni wane wa kutoka Kampuni ya Bima ya *Sanlam Life Insurance* ya Jijiji Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Susan Lyimo, Makamu Mwenyekiti wa *TWPG* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kwamba leo tarehe 12 kutakuwa na semina itakayofanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge saa 7:00 mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas anawatangazia Wabunge kuwa leo kutakuwa na ibada ya misa ya wakiristo wakatoliki mara baada ya kuahirishwa Bunge katika ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili. Aidha Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki ibada hiyo, ya misa pia misa hiyo itakuwa na wanakwaya ya Mtakatifu Antony Kwapandua kutoka Parokia ya Mtakatifu Gema, Galagain Nkhungu Dodoma, wote mnakaribishwa. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018
(The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018)**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na mijadala, tunaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji, ajiandae Mheshimiwa Mwambe.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya mwanzo kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Kipekee na kwa udhati kabisa napenda kabla ya yote kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mpango kwa kazi nzuri sana ambayo amelitendea Taifa hili na historia itakuandika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kipekee nikupongeze kwa hatua ulizochukua kushughulikia kadhia ya makontena ya Mheshimiwa Paul Makonda, Dar es Salaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makonda hawa ndio viongozi ambao Mheshimiwa Rais anaowataka, Mheshimiwa Sheria ni msumeno na katika kutekeleza majukumu yako muhimu ya kusimamia fedha za nchi hii hautakiwi kumuangalia usoni yoyote anayevunja sheria za nchi katika kusimamia kodi za wananchi. Kwa hiyo, kitendo chako kitabakia katika historia, alijaribu kuwachezea wengine, lakini alichezea vyeupe amekutana na cheusi kimemtia doa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu hoja iliyo mbele yetu na kwa kweli hoja hii ni muhimu na imeletwa wakati ni muafaka ingawa imechelewa kidogo. Naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani juu ya hotuba yao waliyotoa kuhusu jambo hilo, hali kadhalika naunga mkono hoja ya Serikali katika kuleta jambo hili. Kwa hiyo, katika hili niko pamoja na ninyi kabisa, kabisa, kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nilichosema ni kwamba tumechelewa kuleta hoja hii kwa sababu ilikuwa ni muda mrefu wako tuliotoa maoni na kuona haja ya Serikali kuingia katika ubia na sekta binafsi ili kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Lakini kwa wakati huo hatukupata nafasi ya kusikilizwa vyema ila sasa Serikali imeliona jambo hili zuri na tunashukuru sana na tunaiambia Serikali ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunga mkono hoja za Serikali mpinzani anayejielewa upinzani sio kupinga kila kitu.

Mpinzani makini hapingi kila kitu, lakini mpinzani makini hakubali kila kitu, lazima kuwe na uchenjuwaji wa kujua chenye maana kifuatwe na kisichokuwa na maana kiachiliwe mbali. Nalisema hili kwa sababu katika siku za karibuni inajengwa dhana kwa wananchi kwamba sisi wapinzani tunapokataa hizi bajeti za Serikali inakuwa ni hoja ya kwamba mpaka maendeleo wananchi wetu hawastahiki kuyapata kwa sababu tunapinga bajeti ya Serikali, jambo ambalo kila mwenye dhana hiyo upande wenu Serikali mnafanya dhambi kwa Mungu na ni kosa kubwa sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwi maana yoyote ya kwamba inapoletwa hoja, kwa mfano, kwenye bajeti tunapokataa bajeti yenu. Tunapoikataa bajeti ya Serikali kwamba sisi tumekataa kila kitu, sio sawa, yako mambo tunayoyakubali lakini mfumo wa bajeti yetu katika kuitisha, katika kupiga kura hautupi nafasi ya kupembua unayoyakubali ni yapi na unayoyakataa ni yapi. Ukikubali unalazimishwa kukubali yote na ukikataa unalazimishwa kukataa yote. Kwa hiyo, kama kuna watu wanaendelea huko kuwaambia wananchi kama wanaochagua wapinzani nchi hii hawafai kupewa maendeleo... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Jielekeze kwenye hoja, twende kwenye hoja. (*Makofi*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo si dhana sahihi, haiwezi kuletwa bajeti inamkamua mtu. Mfano katika bajeti tulichangia tukasema umeme ZECO tunaonewa Wazanzibar lakini ikapitishwa hivyo hivyo, sasa unaletewa bajeti unasema ndiyooo maana yake nini ulichokitetea? Ulichokitetea ni nini, kwa hiyo, hili lieleweke kwamba, tunaungia mkono suala hili la hii sekta ya ubia wa sekta ya Serikali na sekta binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kusema hivi, kwamba katika kukubaliana na hili Serikali iwe makini katika kuingia mikataba na hawa wawekezaji ambao tutaingia nao ubia katika suala hili. Makosa mengi yaliyofanyika ni wakati wa kuingia kwenye mikataba, tunakuwa hatuko makini kiasi

ambacho baada ya muda mfupi nchi yetu inaingia katika majanga makubwa kama ambayo yako sasa hivi huko duniani yanatokea. Kila kesi zinazokwenda katika mahakama za kimataifa tunapigwa, tunapigwa na makosa hayo mliyafanya ninyi wakati wa kuingia kwenye mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tunapofikia katika hali hii na kutaka kujinasua, naomba sana uwepo umakini wa hali ya juu sana. Naishukuru Serikali yetu kwa kuona sasa iko haja ya kujiondoa na ile dhana ya kujifanya Serikali ya Mungu wa Kibani. Mungu wa kibani ana mikono nane lakini hakuna hata mmoja unaoshika, yote ipo tu, kwa hiyo sasa...

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Jamani mie nipo baniani usiseme hivyo. (*Kicheko*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wameona haja ya kuiweka sekta ya binafsi ili kusaidia uchumi wetu, kwa hiyo, naomba tuondokane na hiyo dhana ya mikono nane lakini ambayo haishiki. Lakini katika hoja hii hii tulipitisha sheria hapa katika Bunge ya kwamba kesi zote zinazohusu wawekezaji zitaendeshwa ndani ya nchi yetu. Hili jambo litawapa wakati mgumu sana wawekezaji wenye mitaji mikubwa kuingia katika sekta hii kwa kuhofia mahakama zetu na uendeshaji wa kesi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili suala liangaliwe sana, haitatoa fursa nzuri ya kufanya wawekezaji wa nje waone hadhi kwa sababu watakuwa wana wasiwasi wa kuona kwamba hawatapata haki katika masuala ya kisheria na izingatiwe kwamba nchi yetu imeingia mikataba mbalimbali ya kuridhia ya kuendesha mambo yetu inapofikia mashtaka katika Mahakama za Kimataifa. Kwa hivyo suala hili halitawapa nafasi nzuri ya kuona kwamba iko haja ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilichangie ni hili sharti mliloliweka katika

muswada huu wa kuona kwamba wawekezaji lazima fedha zao waziwekeze katika Benki Kuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia hili mliangalie tena na kwa umakini kwa sababu mwekezaji, hili maana yake labda mngetupa uzoefu mmeli-*quote* wapi? Au ni nchi gani ambazo zimeingia katika sekta kama hizi mmeona wao wamewawekea masharti haya na yamekuwa ni muafaka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo liangalieni, tunapoweka masharti makubwa na wao ndipo wanapoona vikwazo nya kufikia lengo la kuwekeza katika nchi yetu. Sioni umuhimu wa hoja hii ya kuwataka wawekezaji lazima waweke fedha zao katika Benki Kuu yetu. Muwape uhuru wa kuamua na mabenki ya kibiashara yako mengi wao waamue na wawe huru wa kuamua ni wapi watawekeza fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nadhani ni jambo jema na binafsi naunga mkono, kama nilivyosema hoja hii kwa sababu ni matumaini yetu kwamba sasa tunafikia mahali ambapo tunapalenga, na tutaondokana na hii kuwa mionganini mwa nchi za Kiafrika ambazo kila siku tunaenda kubembeleza mikopo kutoka China. Mikopo kutoka China tunaiona athari zake. Kwa hiyo, tutumie fursa hizi zilizopo katika nchi yetu ili kuwekeza na kuwavuta wawekezaji ili wawekeze katika sekta hizi na tuondokane. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mfano ambalo naona ni nzuri sana, mfano barabara kutoka Chalinze mpaka Dar es Salaam. Ingawa sasa tayari Mbunge mmoja aliongea kwamba tayari Serikali imeshajitokeza kuanza kujenga barabara sita mpaka Kibaha, sehemu ambayo ni muhimu sana kutoka Dar es Salaam mpaka Chalinze ingepata kuanzia na hii *private sector* ikaanzia Chalinze mpaka Dar es Salaam baada ya kuanza kuichokonoa kidogo kidogo kiasi ambacho mwekezaji ataona pale patamu pameshaliwa amebakishiwa pale pachungu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vema muangalie kwa makini fedha zetu zitasaidia katika mambo mengine mengi sana na haya mambo ambayo yanaweza kutekelezwa na sekta binafsi kwa kuingia ubia ni mambo ambayo yataifanya Serikali iwe *stable* katika pesa ndogo tunayoikusanya twende kwenye mambo mengine. Nchi nydingi zilizofanya katika mfumo huu zimeendelea na zimepata manufaa makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nirudie kusema nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na nakuambia uzi ni huo huo, mbane Makonda mpaka mwisho ili haki ipatikane, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda anaomba kuwatambulisha wageni wake kutoka *Tv* ya POA ambayo inatoka Dar es Salaam, karibuni. Mheshimiwa Mwambe. (*Makofi*)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia...

MWENYEKITI: Ajiandae Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada uliopo mbele yetu leo unahusiana na sheria ya masuala ya ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. Tumeletewa hapa muswada mbele yetu, lakini ukiangalia historia ya marekebisho ya muswada huu, hii ni mara ya tatu muswada huu umekuwa ukiletwa lakini Bunge hili halijawahi kuelezwza kwa kina ni miradi mingapi sasa hivi inayofanywa kwa ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye kitabu cha Kamati ukurasa wa nane, kwenye ukurasa wa nane kwenye kitabu cha Kamati wanaongelea habari za *blueprint* na nia ya kuleta *blueprint* ilikuwa ni kuhakikisha wana-sort au wana-solve matatizo yaliyoko kwa hawa wawekezaji wanaokuja kwetu na pamoja na watu wenye viwanda na wengine na hii inasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nia ya *blueprint* ilikuwa ni kuondoa milolongo mbalimbali ambayo kimsingi ukienda...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge muswada huu unakwisha mchana, naona mnaanza kutoka toka tutaanza kuandika majina sasa hivi. (*Kicheko*)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, najua unalinda muda wangu pia. Ukienda kusoma huu muswada wenyewe mbele yako hapo ukurasa wa sita kifungu cha 2(a) wanasesma; "*Notwithstanding the subsection one, the Minister may exempt procurement of unsolicited project from competitive tendering where it meets the following criteria.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye *blueprint* walikuwa wanataka kuhakikisha tunaondoa kabisa matatizo ambayo hawa wawekezaji wamekuwa wakiyapata pamoja na *frustration* zao. Lakini wanaleta muswada wanaonesha kama hawataki kutambua vitu ambavyo viko kwenye *blueprint*. Wanasesma kwamba *the project shall be of priority to the government at the particular time and broadly consistent with the government strategic objectives*. Sasa tunaposema *strategies objectives* bila kuzi-*define* moja kwa moja kwamba hizi ni zippi halafu tunataka wawekezaji wawe wanakuja kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kimsingi kuna sehemu unazidi kwenda hapa chini wanaongeza, wanasesma; "*the private proponent does not require government guarantee or any form of financial support from the government.*" Sasa hii ni kuwachanganya hawa watu, tunaposema ni *PPP* maana yake ni ushirikiano katika Serikali na sekta binafsi. Sasa Serikali haiko tayari kutoa pesa kwenye baadhi ya miradi kwa ajili ya uendeshaji wake na leo tunataka tualike hawa watu wakati tulikuwa tukiwa-*frustrate* kila mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu kuangalia hapa tumeuliza swali linalohusiana na suala la reli ya Kusini ambayo ni reli inayoanzia Mtwara Bandarini na kuelekea mpaka

Mbambabay, pamoja na Mchuchuma pamoja na Liganga. Hii ndio miradi ya kipaumbele ambayo kama kweli walikuwa na nia njema ya kuhakikisha yanafanywa kwa *PPP* wangeanza na hiyo miradi. Kwa sababu umuhimu wa hii reli ni kutuwezesha pia sisi kuweza kusafirisha chuma kutoka hayo maeneo kutokea mitaa ya Songea kuleta Mtwara Bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuma hii tungeweza kuiiza nje tukapata pesa ya kigeni na kugharamia miradi yetu mingine. Lakini matokea yake sasa hivi tumekuwa tukitumia hela nydingi sana tunatumia *forex* kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa wakati tungeweza kuanza na miradi ya kipaumbele kuwashawishi wawekezaji kuwawekea mazingira bora ya uwekezaji badala ya kutaka kuleta *frustration*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu nadhani nia hasa ya hii ya marekebisho ya sasa hivi yalikuwa yanalenga kifungu cha 47(7), kifungu cha 53(2), kifungu cha 56(1) kifungu cha 7, kifungu cha 57, 61, 62 na wameleta pale kwa makusudi kabisa wanasema Bungeni taarifa ya uhamisho wa fedha, taarifa ya matumizi, taarifa ya utekelezaji, taarifa kuhusu misamaha ya kodi na taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi sita badala ya robo mwaka kama ambavyo ilivyo sasa hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nia yao hasa ni kutaka kuona kwamba tunapata hizi taarifa kila baada ya miezi sita, kwa nini sio baada ya miezi mitatu kama sheria inavyotaka, kwa nini sasa? Waziri atakapokuja aje atueleze kwamba wameamua kuongeza muda lakini sababu yao ya msingi hasa ni nini? Kwa kufanya hivyo tunakwenda kuwavutia wawekezaji au tunakwenda ku-*frustrate* zaidi *industry*. Kwa hiyo, marekebisho yanapoenda kufanywa lazima tuone yanakwenda kulenga jambo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi sana hapa, tunarudi sasa kule chini kabisa tunasema kwamba mwanzoni ilitangazwa *PPP* tunatafuta wawekezaji kwa ajili ya barabara ambayo ingeanzia Bandari ya Dar es Salaam

kwenda mpaka Mlandizi kama mchangiaji aliyepita hapa alivyosema, lakini matokeo yake sasa hivi Serikali wameamua kutumia pesa nyingi tena za kwake za ndani kadri wanavyotueleza, kwa sababu mara nyingi tunaona wanataja pesa za ndani halafu mwisho wa siku wanakwenda kukopa ili kugharamia barabara ya Kimara mpaka Kibaha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndio kipande ambacho Serikali wangeweza kupata fedha nyingi zaidi na ni sehemu ya kuweza kuweka vivutio. Kwa hiyo, wameachana na ule mradi wa awali wa kupitisha barabara kule Chamazi kuileta pale ambayo ingepunguza kuileta foleni na kinachosababisha haya mambo yote yatokee ni kwa sababu tu Serikali haitaki kufanya mahusiano mazuri na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanakuwa *frustrated* sera zetu haziko *straight* kuonesha nini tunataka kiasi wawekezaji wanakuwa wakipata uoga kuja nchini kuwekeza kwa sababu muda wowote yanaweza yakatokea mabadiliko kwa sababu hiki kitu ni kama kitu cha *one men show*, mtu mmoja anaamua kufanya wakati wowote anaotaka yeeye na haya mambo yanatokea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina-*frustrate* sana wawekezaji wetu hata kama tutarekebisha hapa sheria mara mia moja, bila kuileta ile *Principle Act*, tukaona kimsingi nini tunahitaji sisi kukifanya inaweza isiwavutie sana wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha kabisa na tuelekee pale mbele, sisi kwenye ripoti na taarifa yetu ya Kambi Raskmi ya Upinzani tumeeleza pale wazi kwamba kama Serikali ina nia njema ya kutaka kuona wawekezaji hasa hawa wa kushirikiana *public and private sector* wanakuja kufanya kazi kwa pamoja cha msingi cha kuangalia kwanza ni kanuni za uwekezaji, mazingira bora ya kuhakikisha hawa wawekezaji wanapokuja wanalindwa na mikataba yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku ndani tunaongeza sehemu nyingine ukisoma kwenye huu muswada uliopo hapa mbele yetu wanasema hata hizo kesi zitakazofanyika *arbitration* kama mambo yatakuwa yameshindikana kule ndani zipelekwe mahakama za hapa hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni mwekezaji gani alete pesa yake nchini kwetu halafu yanapotokea kutokuelewana kati ya mwekezaji pamoja na Serikali na hizi kesi bado zizidi kusikilizwa hapa hapa ndani. Ni kesi ngapi ambazo hazijaenda vizuri tunajua, sheria yetu sasa hivi haijasimama vizuri maeneo mengi. Kwa hiyo, tunawatengenezea mitego kiasi kwamba wawekezaji wetu sisi wanashindwa kuja kwa sababu wanafikiri wanakuja kupoteza pesa zao hapa. Tumeona kwa mfano kuna mradi sasa hivi ukienda jimboni kwangu kuna mradi pale wa kuchimba madini ya *graphite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji walikuwa tayari kabisa kuja kuanza ile kazi, lakini wamekuwa *frustrated* baada ya kuamua sasa kubadilisha ile sheria ya madini, yale masuala yanayohusiana na makinikia ambayo kwa kweli haijafanikiwa kokote, sana sana wale wawekezaji wanapokutana kwenye *round table* zao kwenye hizo nchi zao wanapajaribu kukusanya mitaji wanaulizana unakwenda kuwekeza nchi gani. Wakiambiwa wanakwenda kuwekeza Tanzania wanakuwa *frustrated* kwa sababu sheria zetu zimekuwa zikibalika kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuja hapa sheria inakuwa *vague*, mwisho wa siku wanakwenda kuwabana wawekezaji kwa kutumia kanuni ambazo zinakwenda kutengenezwa kwa mamlaka aliyopewa pale Waziri. Kwa hiyo, niombe tu kwa nia njema kabisa kwamba tuangalie namna bora tulete hizo *principle act* badala ya kufanya *amendment* vipande vidogo vidogo kila siku kwa sababu watu wanaweza wasio *proper correctors* wa hivi vitu mwisho wa siku inakuja kuwabana kwenye maeneo ambayo wanashindwa kwenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema hizi *unsolicited project* lazima hapa tuwe wazi kabisa, Serikali inataka kujivutia upande wake tu bila kuangalia hata hawa wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza wao wanunuifaika vipi. Hii ni namna ya kuwatisha hawa wawekezaji, tumeona kuna maeneo mengi ambayo wawekezaji wamekuja, lakini mwisho wa siku wameishia ku-withdraw. Tunaambiwa sasa hivi kuna wawekezaji wa viwanda zaidi za 53,000; kuna watu wameenda *TIC* wameenda kuomba leseni za kutengeneza viwanda lakini tu wakisha-*register TIC* sisi tunawaita moja kwa moja wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatupeani *actual fact*, hatupeani *figures* hasa zinazowahusu hawa wawekezaji, yaani hatupeani takwimu sahihi kabisa kuhusiana na masuala ya wawekezaji. Na hii inawatisha kwa sababu ukienda kwenye mtandao wetu, ukiangalia masuala ya kiuchumi *against* haya masuala ya uwekezaji utakuta ni vitu viwili tofauti kabisa. Hawa wawekezaji wanapotaka kuja lazima wawe wanaangalia hivi vitu viwili na kufanya mlinganisho kwamba uchumi wa nchi hii ukoje, wawekezaji mazingira yao yakoje. Lakini pamekuwa na milolongo mirefu wawekezaji wengi wanashindwa kuja nchini, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, unga mkono hoja.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunga mkono hoja maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Hawa Mchafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Nagu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na wasaidizi wao wote kwa kutuletea muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kama walivyosema wachangiaji wengine wengi, ni vigumu sana mwekezaji yejote makini kwenda kuwekeza mabilioni ya shilingi kama hana uhakika na usalama wa pesa zake. Kwa hiyo, mabadiliko haya ya sheria yalikuwa ni ya lazima kwa sababu wawekezaji wetu wengi duniani ni wawekezaji ambao pesa siyo za kwao, wanazipata kwenye mabenki, wanakopa. Kwa hiyo, anapokuja hapa bila kuwa na uhakika na usalama wa pesa zake hawezu kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo nilitaka nianze kwa taarifa ya Kamati kwenye ukurasa wa tisa ambapo ukienda kwenye *item* namba 2.2 utagunduakwamba mwaka 2017 tulipitisha hapa sheria ambayo ilikuwa inaruhusu Halmashauri zetu kubuni miradi ya kimkakati na kuwasilisha Serikalini na kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibuni hapa tulipata taarifa kwamba ni Halmashauri chache sana ambazo zilifanikiwa na moja ya sababu kubwa ambayo ninaiona ni kukosekana kwa ujuzi kwenye Halmashauri zetu na siyo kwenye Halmashauri peke yake. Kwa sababu kama Halmashauri zetu na Wizara zingekuwa na wataalam wa kutosha wangeweza kutoa msaada huu kwenye Halmashauri zetu. Leo tungekuwa tunapata tathmini ya hatua kubwa mbele tulioipiga kwenye sheria ambayo tuliiweka, lakini matokeo yake tunaendelea kuwa Halmashauri mbili/tatu ambazo zimetekeleza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana mkono kabisa na Kamati kwamba iwepo programu maalum ya kuwawezesha wataalam wetu ili wapate uwezo wa ku-*plan* hii miradi, kuisimamia, lakini pia kutengeneza maandiko ambayo yatatupeleka kwenye utekelezaji wa sheria hii bila kuwa na ubabaishaji. Kama tukiendelea bila kujenga uwezo, tatizo tulilokwa nalo mwanzo la kuwa na watu kwenye ofisi ambao hawawezi kufanya upembuzi yakinifu na pia hawawezi kufanya maamuzi, litaendelea, kwa hiyo, naungana mkono na Kamati.

Naomba sana kwamba katika hatua hii Mheshimiwa Waziri atafute namna ya kufanya *investment* ya kutosha ili kupata watu ambao wataweza kuisaidia Serikali kwa sababu tunaweza kuitisha sheria nzuri, lakini mwisho wa siku sheria ikaendelea kubaki kwenye Kamati na isiweze kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi sana ambazo pamekuwa na sheria hii na hasa katika nchi ambazo zimetolewa mfano hapa, zipo sababu nyingi ambazo zimesababisha ikaonekana kwamba Sheria ya *PPP* nayo haifai. La kwanza, ni mazingira ambayo Serikali itaweka. Inawezekana kabisa Waziri wa Fedha akawa na nia njema ya kutaka wawekezaji waje na wabia waje, lakini hayuko peke yake, ana watu wengi ambao lazima wafanye kazi pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaenda kwa Waziri wa Fedha, yuko sawa, wakaenda watu wengine wa Mazingira wakakwamisha, wakaenda watu wa Ardhi wakakwamisha, wakaenda watu wa Mambo ya Ndani wakakwamisha. Kwa hiyo, ni lazima hizi timu zote zifanye kazi kwa pamoja ili wawekezaji wanaokuja wenye nia njema ya kufanya kazi na Serikali waweze kuona kwamba nia kweli tumedhamiria kutumia sheria hii kuleta mabadiliko makubwa katika uwekezaji na katika uchumi na faida ziko nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukitumia pesa nyingi sana za kwetu kufanya miradi mingine. Iwapo tutapata *partners*, maana yake ni kwamba tutaelekeza pesa zetu za ndani kwenye maeneo ambayo tunadhani wawekezaji hawaoni faida, kwa sababu hakuna mtu amekwenda kuwekeza sehemu ambapo hawezikupata faida. Jambo hili ni muhimu sana, kwa hiyo, Serikali yenye ni muhimu kuwa imojiandaa lakini kuwaandaa wawekezaji waweze kufahamu kwamba ni maeneo gani wakikwama, wakimbilia wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ni kitu muhimu sana kwenye suala hili. Nataka kutoa ushauri kwamba

pawepo na kanzidata (*database*) ambayo itaonesha kutokea kwenye Halmashauri zetu/kwenye Manispaa ambayo itatusaidia kufahamu mtu akiwa duniani popote pale katika nchi yoyote duniani aweze kujuu nikienda Tanzania, maeneo ya *priorities* ni haya hapa ambayo unadhani naweza nikaenda kuwekeza. Isitokee mahali unakuta sehemu hii wanafahamu hiki, sehemu hii hakuna muunganiko wa mawasiliano, tutajikuta kila siku na tunaanza upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kisiasa ni muhimu sana katika suala hili. Naomba tu niseme vizuri kwamba tunategemea sana kwamba kauli na msukumo wa Mawaziri wetu tuweze kuwasaidia wawekezaji. Tunalo tatizo sana kwenye maeneo yetu huku chini kwamba inawezekana huku mna-*push* suala liende, lakini kwa sababu watendaji wetu huko chini hawaoni faida na kwa sababu watu wengi wamezoea kupata *commission*, wanaona kwamba suala hili halina faida sana kwao, wakalikwamisha bila sababu. Kwa hiyo, tunataka sana Mheshimiwa Waziri mkono wake huu na wasaidizi wake huko chini uweze kusukuma mambo haya yaweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la mikataba. Nchi nyingi ambazo zimepata shida kwenye mikataba, haikuja kwa bahati mbaya, ni kwa sababu hapakuwa na *transparency*. Watu wengi wanaopelekwa kuingia kwenye mikataba aidha uwezo wao ni mdogo au ni mkubwa sana, kwa hiyo, matokeo yake badala ya kuona maslahi makubwa ya nchi wanajikuta wanaweka zaidi maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala linafanyikaje? Anaweza kuja mwekezaji hapa leo, anataka kuwekeza shilingi bilioni 100 na anataka kufanya *payback* ya mradi ule ule labda miaka 10, lakini anayekwenda kuweka mkataba akasema wewe fanya hiyo miaka 20 na uhakikishe mradi huu unaghari mu shilingi bilioni 200. Matokeo yake mradi huu unaonekana tena hauna faida kwa wananchi au una

gharama kubwa. Kumbe tatizo kubwa hakukuwa na transparency kwenye mkataba. (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Hawa halafu Mheshimiwa Dkt. Nagu ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia muswada huu wa ubia katika sekta binafsi na sekta ya umma. Awali ya yote napenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta marekebisho haya ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kusoma tafsiri ama maana tofauti ya hili neno *PPP* lakini pia ukiangalia madhumuni ya mapendekezo ya sheria hii, huoni moja kwa moja ni kwa namna gani mradi wa Daraja la Kigamboni kwamba ni mradi wa *PPP*. Pia mabasi yaendayo kasi ukiangalia hasa tafsiri ya *PPPhuioni* moja kwa moja. Uki ja pia kwenye ule mradi uliokuwa mwanzoni uanzie Kigamboni uje Ubungo mpaka Mlandizi - Chalinze lakini kwa sasa kwa namna inavyoenda pia hajjieweki waziwazi kama ni mradi wa *PPP*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nisome madhumuni au kusudio la kuletwa marekebisho haya. Nikianzia hapa inasema kwamba juu ya madhumuni mengine, lakini hapa anasema; "Aidha, muswada huu unakusudia kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya *PPP* mamlaka ya kisheria ya kuidhinisha miradi ya ubia katika sekta binafsi na sekta ya umma kwa lengo la kuimarishe utekelezaji wa miradi ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napenda sana kuipongeza Serikali kwa kusudio hili. Kiukweli tuna miradi mingi sana na mikubwa sana nchini kwetu ambayo kimsingi Serikali

ikisema ifanye miradi hii yote kwa pesa yake yenyewe binafsi hatutakaa tumalize ama tutaimaliza kwa kuchelewa sana ukililinganisha na nchi nyingine duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi kwa mfano wa reli ya katiba wenye kilometra takribani 2,700 ukijumlisha na matawi yake ambayo kimsingi tunajenga kwa fedha za ndani. Pia tuna mradi wa reli ya kwenda Kusini na Kaskazini, upanuzi wa viwanja vyatia ndege, upanuzi wa bandari, ujenzi wa vivuko na ujenzi wa meli. Kwa hiyo, ukichukua miradi hii yote ukisema tusubiri Serikali itekeleze kwa fedha yake binafsi tutachelewa na tutaachwa na wenzetu ambao kimsingi hapo awali wao tulisha nyuma, sisi tulikuwa mbele, lakini kwa sasa wametuacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi kama *South Africa*, India, Brazil na China wenye ukiangalia uchumi wao na muonekano wa nchi zao wametuacha mbali sana. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuona huo umuhimu wa kuweza kuleta marekebisho haya ya sheria. Umuhimu wa suala hili na hata tukiangalia kwa upande wetu wa bajeti, haitakaa ituathiri kibajeti. Kwa sababu gani nasema hivyo? Kuliko kutenga bilioni kadhaa *at once* kwa mradi mmoja, ni vema mradi huo tukauingiza kwenye masuala ya *PPP*. Halifu kitu tutakachokifanya, kila mwaka wa bajeti tuwe tunatenga fedha ile kidogo kidogo mpaka kufikia ile miaka aidha, 20 ama 30 tuliyokubaliana ya utekelezaji wa mradi ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunajikuta kwamba mambo yetu mengine ambayo yanawavutia wawekezaji tunayafanya na yale mambo ambayo wawekezaji hawapendi kupeleka fedha moja kwa moja, pia tunakuwa tunafanya. Kwa hiyo, masuala mazima ya *PPP* ni masuala muhimu sana kwa Taifa letu hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine napenda tu kuishauri Serikali, amesema ndugu yangu Mheshimiwa Kanyasu na mimi nitapenda kukazia hapo. Hii Sheria ya *PPP* tulikuwanayo miaka nane iliyopita, leo yameletwa marekebisho. Kimsingi unaona kabisa hatujawahi kufanikiwa

kwenye mradi wa *PPP* na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri kwenye taarifa yako mifano uliyotoa ni Kigamboni na barabara ziendazo kasi ama mabasi yaendayo kasi, huoni moja kwa moja ile maana hasa ya mradi wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kimsingi kwenye *PPP* hatukufanikiwa. Sababu ambazo zimepelekea kutofanikiwa ni pamoja na kutokuwa makini katika kuingia hii mikataba. Tumekosa umakini mzuri katika kuingia hii mikataba ndiyo maana tumejikuta tunakosea ama tunashindwa mradi, tunafanya namna ya kuingia miaka 90 ndiyo huo mradi wawekezaji watuachie sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kila mradi tunaweza kuingia nao kwenye *PPP*. Kwa mfano, tukisema miradi ya barabara, barabara *life span* yake ni miaka 30. Kwa hiyo, tunajengewa barabara katika tafsiri kwamba mwekezaji atoe huduma na aweze kurudisha faida yake na baada ya hapo airudishe kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitu kama barabara, baada ya miaka 30 au 20 inakuwa tayari imeshachoka, kwa hiyo, ndicho hicho ninachozungumzia umakini katika *design*. Watu wetu tutakaowapa hili suala au watakaosimamia haya masuala, mbali ya kwamba watatakiwa kujengewa uelewa, pia mbali ya kuwa makini katika masuala ya mikataba, namna ya kuiingia ni muhimu kwenye suala la *designing* wakawa makini kweli kweli, siyo kila mradi tutakaoweza kuuingiza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililokuwa nataka kulizungumza, nakubaliana na wale wote waliosema kiukweli tumechelewa kufanya marekebisho ya sheria hii. Ni kweli tumechelewa kwa sababu uzuri wa miradi ya *PPP* vihatarishi vyote vinabebwa na mwekezaji. Pia tuna *chance* ya kuchagua namna ya ule mradi tunapenda uweje ama uonekanaje? Kwa hiyo, siyo suala la kukaa nalo mbali au siyo suala la kulala, ni suala la kulichangamkia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia umuhimu mkubwa ambao unakuwepo hapa katika masuala mazima haya ya uwekezaji wa *PPP*, mwekezaji anawekeza katika lengo la kufanya biashara. Mbali ya hapo atalipa kodi kwa Serikali yetu, atatoa ajira kwa vijana wetu na baada ya miaka kadhaa atarudisha ule mradi kwa Serikali yetu, inabaki kuwa mali ya Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala cha msingi ninachozungumza hapa, hatuhitajiki kulala, tunahitajika kuwa *faster* katika suala hili, kwani wenzetu wametuacha mbali sana. Kikubwa zaidi hapa, lengo la mwekezaji kufanya biashara ambalo atakakuwa nalo *whether* kwenye mradi wowote atakaouanzisha, fedha zitarudi kwa Serikali kupitia kodi, lakini pia ukiacha masuala mazima hayo ya kodi, kama nilivyozungumza suala la ajira, suala la utoaji nafasi mbalimbali kwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri.
Mheshimiwa Dkt. Nagu.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika muswada huu muhimu wa uwekezaji hasa marekebisho ya Sheria ya *PPP*. Napenda ku-*declare* kwamba kwa miaka minne nilikuwa Waziri wa Uwekezaji na Uvezeshaji ambapo nilikuwa nasimamia hii sera na Sheria ya *PPP*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba tulikuwa wote kwenye hii Wizara, amesaidia sana kuleta marekebisho haya, lakini vilevile napenda kukumbuka jinsi Dkt. John Mboya alivyoifanyia kazi sana sheria hii na leo amekuja na

marekebisheso alivyomshauri Waziri wake, bila kumsahau Naibu Waziri na Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nasimamia sheria hii, ilionesa changamoto kubwa ambazo kwa maoni yangu kwa kiasi kikubwa zitakuwa zimeondolewa na haya marekebisheso ambayo ameyaleta Mheshimiwa Waziri. Madhumuni ya marekebisheso haya yameainishwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri kwamba lengo la muswada huu ni kufanya marekebisheso ya sheria ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia na pia kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi ya *PPP* ili kurahisisha uibuaji, uidhinishaji na utekelezaji wa miradi ya *PPP*. Vilevile muswada unakusudia kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha mamlaka ya usimamizi ya utekelezaji wa sera na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa Waziri, Waziri wa Fedha alikuwa na mamlaka na Waziri wa sekta ile ambayo inaibua mradi alikuwa na mamlaka. Sasa kinachohitajika hapa ni uratibu au *coordination* kwa sababu watu sasa wamepunguza majukumu ya Waziri wa Uwekezaji. Kwa hiyo, watakuwa wamebakili Waziri wa Fedha na wa sekta ile ambayo inaleta mradi wa ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeondoa urasimu ambao upo. Na mimi nashukuru sana kuona kwamba tumeponguzza urasimu kwa kiasi kikubwa, hivyo muda utakaotumika na tofauti zitakazokuwepo zitakuwa ni chache sana. Vilevile marekebisheso haya yataimarisha usimamizi wa sera na wa sharia na nakumbuka kuna miradi iliyoanzishwa kabla hata ya Sheria ya *PPP* kuanzishwa. Kwa mfano, mradi wa kufua umeme wa Kampuni ya *IPTL*, mradi wa huduma ya maji wa *City Water* Dar es Salaam na mikataba ya huduma ya usafiri wa reli ya kati. Hiyo ilikuwa ni miradi ya *PPP* lakini haipakuwa na sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyoonekana yote haikufanikiwa, ndiyo Serikali ikaamua kuanzisha sera na sheria.

Hii ni sheria ya kusimamia miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi iweze kuwa na maandalizi mazuri na usimamizi mzuri. Kuwepo kwa sheria na sera imeonesha kuwa ikisimamiwa vizuri, kutakuwa na urahisi wa kutekeleza miradi ya *PPP*. Kwa hiyo, nataka nikumbushe alichosema Balozi Kamala kwamba kuna *models* tano za kuweza kutekeleza *PPP*. Kuna ile ya *design, financial, operate* na *ku-transfer*, kuna ya *ku-design, finance operate* bila *ku-transfer*, kuna *design, build, operate and transfer*, kuna *equity partnership* na kuna *facilities* za *ku-manage projects*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu katika marekebisho haya tuone kwamba ni *model* ipi ambayo inafaa kwa kila mradi. Kwa hiyo, suala la kusimamia ni muhimu sana. Vilevile *PPP* pamoja na maboresho au marekebisho haya itaongeze kasi ya uwekezaji kupitia ubunifu wa pande zote mbili, sekta binafsi na sekta ya umma kutumia ubunifu, teknolojia na matumizi ya mitaji katika sekta binafsi. Utaratibu wa *PPP* utaharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hudumu za umma kwa sababu bajeti ya Serikali ni wazi haitoshi na mahitaji ya maendeleo kwa nchi yetu ni makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia uwekezaji huu wa *PPP*, wananchi watapata ajira. Vilevile zaidi ya ajira, mapato ya Serikali yataongezeka kupitia kampuni hizo ambazo zitatokana na *PPP*. Hata hivyo ufanisi wa kutoa huduma bora na gharama nafuu itakuwepo. Serikali itaokoa fedha za bajeti kupitia miradi ya *PPP*. Siyo fedha tu ambazo tunazipata kwa sekta binafsi kuna utaalam amba Serikali hauna, lakini sekta binafsi unao. Tukitumia utaalam huu vizuri, miradi itaendeshwa vizuri na kwa hiyo, nina hakika kwamba tutapata manufaa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuwa miradi inayoandalowi ikiwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa viwanda vya madawa kwa utaratibu wa *PPP*, mradi wa ujenzi wa hosteli ya *CBE* na mengineyo hasa mimi nafkiria miradi ya miundombinu

inaweza ikasaidiwa kwenda kwa kasi kubwa kama *PPP*nayo itatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatua nzuri sana hapa tumeona kuwa Serikali imedhamiria kwa kuleta marekebisho hayo, naomba marekebisho hayo tuyapitishe ndugu zangu. Kwa sababu tukipitisha, maendeleo yetu yataenda kwa haraka na tutakuwa tumempa Rais wetu ambaye anataka maendeleo kwa haraka yaweze kwenda kwa haraka zaidi. Sioni kwa nini mtu asite kukubali marekebisho ambayo yanaleta maboresho. Ili utaratibu uwe na manufaa kwa Taifa letu, lazima tukabiliane na changamoto kuu za utekelezaji. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 nilipokuwa Waziri wakati nasimamia *PPP*, nilileta marekebisho ambayo yalianzisha centerya *PPP*na centerhiyo bado ipo. Kwa hiyo, sasa tumeongeza marekebisho, nina hakika mambo hayo yataenda vizuri. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kufanya marekebisho hayo na sasa Serikali inaleta maboresho zaidi kuna umuhimu...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, malizia.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: ...na taasisi kuwa na uzalendo mkubwa na watalam kuwa na uzalendo mkubwa. Kuna watu wanaogopa miradi ya *PPP*kwa sababu wanafikiri wanagawanya mamlaka, manufaa waliyokuwa wanapata binafsi...

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Ahsante.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nitashirikiana na Serikali kufanya yote yafanikiwe. Ahsante sana. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kwenda kwenye *pigeon holes* zenu mkachukue CDza Gazeti la Serikali na mpunguze nyaraka zilizokuwa kwenye *pigeon holes*. Shughuli ya kesho hii ya *heforshe* ambayo ilikuwa ifanywe kesho, imeahirishwa kutokana na *logistics* ambazo bado hazijakaa vizuri. Kwa hiyo, Katibu wa Bunge anawatangazia shughuli ya kesho ya uzinduzi wa hii *heforshe* imeahirishwa.

Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa dakika tano.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kuunga mkono muswada huu wa *PPP*. Vilevile nikianzia katika masuala ambayo yalijitokeza kwa wazungumzaji, niseme tu ukienda kwenye Katiba yetu sehemu ya pili, inazungumzia kwamba malengo muhimu ya mwelekeo wa shughuli za Serikali, ukienda kwenye kifungu cha 9, itakuwa ni ujenzi wa ujamaa na kujitegemea. Nasema hivyo kwa sababu gani? Ni kwamba kila suala ambalo tunajaribu kulifanya ni kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukienda kwenye kifungu cha 20 inazungumzia juu ya uhuru na haki ya mwananchi ye yote yule kuweza kukutana au kushirikiana na watu wengine katika kufanya shughuli zao. Katika kifungu cha 25 kinazungumzia juu ya kazi pekee ndiyo izaayo utajiri wa mali katika jamii na chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu; na kila mtu anao wajibu wa kwanza kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali za uzalishaji mali. Vilevile (b) inazungumzia kutimiza nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji mali ya binafsi na yale malengo ya pamoja yanayotakiwa au yaliyowekwa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo niseme tu kwamba vifungu vyote ambavyo vimeletwa na Serikali vina dhamira hiyo njema kabisa. Vilevile tunatambua kwamba katika *PPP* tunaenda kutumia rasilimali za nchi na za watu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono pia kifungu cha 13 ambacho tumeongeza sasa kifungu cha 25 kinachotambua sheria ambayo ilipitishwa hivi karibuni juu ya utajiri wa nchi. Hivyo basi, napenda kusisitiza sasa, kwa sababu sheria hii imetoa nafasi kubwa kwa wadau mbalimbali kushiriki katika uwekezaji wa *PPP* na hasa kwa hawa wananchi ambaao ni wananchi wa kawaida ambaao pengine tulikuwa tunafikiria siku za nyuma wanaotakiwa kushiriki katika *PPP* ni Serikali pekee au wadau wenyewe fedha nyingi peke yao, nawaomba kutumia taasisi zetu za kitafiti ili waweze kusaidiwa katika kupata michanganuo na kuweza kupata namna bora ya kuingia katika ubia na kuleta faida ambayo itakuwa kwao katika hao wajasiriamali lakini halikadhalika kwa nchi yetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu kuna uzoefu umejitokeza, unakuta pengine wadau au wabia wanaotaka kuja, anasema pengine anataka *government guarantee* au anasema kwamba nimeshapita mahali huku nimeshaona kwamba naweza nikawekeza katika eneo hili. Kwa upande wa Serikali au upande wa yule mtu ambaye anataka kushirikiana naye unakuta hana taarifa za kutosha na hivyo kufanya ule mradi kwa ujumla wake kutokutoa faida za pamoja au kuweza kunufaisha upande mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ilishapata matatizo hayo. Nchi yetu ni mionganini mwa nchi za Afrika zinazozungumza kwamba utajiri wake umetumika kunufaisha nchi nyingine. Kwa misingi hiyo, napenda kuomba taasisi zote zitakazoshiriki katika shughuli hizi za ubia, pia watu binafsi kujielekeza kupata taarifa za msingi kuhusiana na ubia wanaoingia ili kuona kwamba ubia huo unakuwa ni wa haki na wa faida kwa pande zote. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika kuhitimisha hoja iliyopo mezani ambayo inahusu Sheria

ya *PPP*. Mchango wangu nitauelekeza kwenye mambo mawili. Swali la kwanza litakuwa la utatuzi wa migogoro ambalo lilibuliwa katika michango ya Mheshimiwa Halima Mdee na pia Mheshimiwa Khatib Haji naye amejielekeza katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwa na maoni kwamba utatuzi wa migogolo usifanyike kwenye mahakama za ndani, ufanyike kwenye *neutral ground* na Mheshimiwa Halima alitoa mifano ya *ICSID, MIGA* na kadhalika. Pia alisema kwamba tatizo kubwa ni mikataba na kwa kweli siyo mfumo wa utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nitapenda kuligusia ni suala la mfumo wa sheria ambalo hili lilitusimia kwenye mchango wa Mheshimiwa Msigwa. Yeye allizungumza kama mambo matatu hivi kwamba tuna shida pengine katika sheria zetu, masuala ya *sanctity of contracts*, masuala la *clarity of regulatory framework*, masuala ya utatuzi wa migogoro na pia akarejea masuala ya *MIGA* kwamba tumesaini mikataba ya *MIGA* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sheria ya *PPP* ni sheria ya masuala la mambo ya uwekezaji, ni mojawapo ya sheria zinazosimamia masuala ya uwekezaji. Unapozungumzia sheria zinazosimamia masuala ya uwekezaji, yapo matatizo makubwa mawili yanayojitokeza na pengine ndiyo yaliyopelekea baadhi ya Wabunge waliochangia hoja hiyo kutoa hoja walizotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la historia ya sheria hii, sheria hii imepita hatua zipi na hatua zipi mpaka kufikia tulipo sasa hivi? Hapa nazungumza katika sheria hii iko katika ngazi ya kimataifa, ngazi ya kikanda, inakuja kwenye ngazi ya kitaifa na inakuja kwenye ngazi ya mahusiano kati ya wawekezaji pamoja na Serikali. Hilo ni jambo la kwanza ambalo nalionna ni tatizo kwamba hatuangalii historia, haturudi katika historia, hatujipi nafasi ya kujifunza kutoka katika historia.

Jambo la pili ambalo naona ni tatizo, ni kwamba hatuangalii mambo yanayoendelea sehemu mbalimbali duniani na hasa yanayoendelea katika nchi zinazoendelea, katika nchi za Afrika na mwisho Tanzania. Kwa hiyo, tunajenga fikra kwamba haya tunayoyafanya Tanzania ni sisi wenyewe tunayafanya peke yetu, hali siyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kurudi kidogo katika historia, jambo ambalo ni muhimu sana. Ukitungumzia sheria zinazosimamia masuala ya uwekezaji, pamekuwa na mabishano ya muda mrefu, hayajaanza leo kati ya nchi zinazoendelea, kati ya nchi zinazopokea uwekezaji, dhidi ya nchi zilizoendelea na dhidi ya nchi zinazotoa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabishano haya yamekuwa katika maeneo makuu manne; sheria zipi zinapaswa kusimamia ile tunaita *admission of investments*, sheria zipi au misingi ipi inatakiwa kutumika katika *ku-control host states*, zile nchi zinazopokea *investments*; sheria zipi zinatakiwa kutumika katika kudhibiti (*control*) makampuni ambayo yanafanya uwekezaji na pia mwisho suala la nne masuala ya utatuzi ya migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria imekuwaje? Katika ngazi ya kimataifa imeanza kwa kutengenezwa kwa kitu kinaitwa *principles of customary international law* (sheria za mapokeo). Katika Sheria za Mapokeo ipo misingi mingi sana huko ndani yake, lakini itoshe tu kusema kwamba nchi zinazoendelea na nchi zilizoendelea zilibishana sana kuhusu ni zipi hasa au ni ipi hasa misingi ya *customary international law* ambayo tunaikubali wote.

Mojawapo ya mambo yaliyobishaniwa sana tukiongozwa na nchi za *South America* na nchi nyingine za Asia kama Iran na kadhalika kwamba utatuzi wa migogoro unatakiwa ufanywe wapi? Ndiyo maana tukapata kile kitu kinaitwa *Calvo Doctrine*. Nchi za *South America* miaka ile ya 1960 mwanzoni inasema: "utatuzi wa migogoro ya

uwekezaji ifanyike kwenye nchi uwekezaji unapofanyika" nchi zilizoendelea zikakataa. Kwa hiyo, huo ubishani umekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kutokukubaliana sana katika sheria za *customary international law*, ndiyo tuka-move katika hatua nyingine. Nchi zilizoendelea zikaja na wazo la kutengeneza mikataba ya kimataifa, *multilateral investment treaties* na ziko nyingi. Katika eneo hilo pia hatukukubaliana nchi zinazoendelea na nchi zilizoendelea kwa sababu moja kuu, mikataba mingi na ambayo ilikuwa inatungwa kwa wakati huo ilikuwa ina lengo la kumpendelea mwekezaji na kuikandamiza nchi ambayo inapokea ule uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe mifano michache hapa ya mikataba ambayo haikuweza kufanikiwa kwa sababu ilip pingwa na nchi zinazoendelea. Mwaka 1967 nchi zinazoendelea zilitoa kitu kinaitwa *Convection on Protection of Foreign Property*, ilikataliwa na nchi zinazoendelea. Mwaka 1975 iliteuliwa *Code of Contract on Transnational Corporations* ilikataliwa; mwaka 1976 iliteuliwa *Declaration on International Investment and Multinational Enterprises* ilikataliwa; na mwaka 1992 kiliteuliwa kitu kinaitwa *Multilateral Agreement on Investment* ilikataliwa. Zote hizi zimekataliwa kwa sababu nchi zinazoendelea zinafikiri kwamba mfumo huo unatengenezwa kibabe na nchi zilizoendelea kuzigandamiza nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushindwa katika *Multilateral Treaties* ukaja sasa mfumo mpya, *Bilateral Investment Treaties*, hizi nazo zimepingwa sana na nchi zinazoendelea na kwa sababu pia zina masharti ambayo yanatupa shida. Baada ya kuona sasa *Bilateral Investment Treaties* nazo zinapata shida, ndiyo tumekuja kwenye kitu kinaitwa makubaliano kati ya mwekezaji na nchi husika (*State Investor Agreement*). Hizi nazo zimepingwa na nchi zinazoendelea, kwa nini? Kwa sababu ile *agreement* nayo inatengeneza sheria yake peke yake na kwa namna moja au nyingine imezichukua zile *principles* za *customary International Laws* zilizokataliwa na kuziweka kinyemela

kwenye hiyo mikataba. Kwa hiyo, nchi nyngi sasa hivi zinasema tusiweke mikataba, mwekezaji atumie sheria ya nchi ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuje kwenye suala la nini kinachoendelea duniani? Nimesema kwamba tunapokuwa tunazungumza hapa tusijitazame wenyewe, tuangalie nini kinachoendelea sehemu nyingine zote duniani? Katika nchi zote zinazoendelea na katika majukwaa mbalimbali, kuna mijadala inayohusiana na mfumo wa sheria zinazoshughulikia masuala ya uwekezaji na nchi zote zinazoendelea zina msimamo mmoja, haziridhiki na mfumo uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika Bara za Afrika ndiyo mijadala iliyopo. Kwa unyenyekevu mkubwa sana nitaeleza, mimi nimkuwa Mwenyekiti wa ile Tume ya Sheria za Kimataifa za Umoja wa Afrika kwa miaka sita na haya ndiyo yalikuwa mazungumzo siku zote. Nchi za Afrika haziridhiki na mfumo uliopo. Sasa tulichofanya Tanzania ni hatua za kishujaa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakuongeza dakika tano. (*Makof*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tulichofanya Tanzania ni hatua ya kishujaa kweli kweli, ni nchi chache duniani zilithubutu kuchukua hatua hizo kama Iran miaka ya 1950, ilichukua hatua hizo dhidi ya uwekezaji wa Marekani. Walipewa msukosuko mkubwa, walihangaishwa, lakini waliweka misingi tunayoitumia mpaka leo kwenye mambo ya *OPEC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nimalizie kwa *ku-address* ile hoja kwamba twende kwenye *neutral forum*. Tositumie Mahakama zetu twende kwenye *neutral forum*. Na mimi nauliza swalii, hizo *neutral forum* ni zipi? Kuna mtu ye yote anaweza kunitajia hiyo *neutral forum*? Mheshimiwa Mdee

alitaja kuna *ICSID*, kuna *MIGA* na kadhalika. Nani ameitengeneza *ICSID*? Nani ameitengeneza *MIGA*? Ni *World Bank*. *World Bank* ndiyo *financier* mkubwa kwa *investors* wengi. Nani mchangiaji mkubwa kwenye *World Bank*? Swali rahisi tu. Kwa hiyo, huyo huyo ambaye ndio *financier* mkubwa ndiye ametengeneza mifumo ya utoaji haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo mifumo ina matatizo gani? Ina matatizo makubwa sana. Hili liko wazi, limeandikwa na wasomi, wataalam na watu mbalimbali, siyo kutoka nchi zinazoendelea tu, hata nchi zilizoendelea zenyewe hawaridhiki pia. Mfumo huo unadhibitiwa na watu wachache sana. Hii *International Arbitration* inadhibitiwa na watu wasiozidi 50. Hawa ndio *Arbitrators* kwenye kesi zote. Kwa hiyo, wamejipanga na wanajuana, na wewe ukiwa na kesi watakwambia, *choose an arbitrator from the list of arbitrators approved by the tribunal*. Hakuna namna! Huwezi ukapeleka mtu wako hapa akaenda kuwa *arbitrator*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hao unaowaambia wachague, wamepatikana wapi? Mfumo wenyewe haupo *predictable*, tumezoea kwamba katika mahakama nyiningine za kawaida uamuzi unapofikiwa, sheria iko wazi, taratibu ziko wazi. Katika hizi *international tribunals* sheria wakati mwingine haziko wazi, taratibu haziko wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna shida ya *arbitrators*, hawa kuegemea upande wa *investors*, hilo liko wazi, hatusemi Tanzania peke yetu, hapana. Watu wengi walio-*observe* mambo yanavyofanyika katika *international arbitration* wameeleza wazi kwamba *arbitrators* wazo *biased*. Nawe kaangalie *record* ya nchi zilizokwenda kwenye *arbitration* kwa mfano *International Center for the Settlement of the Investment Disputes (ICSID)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zinazoendelea zimeshindwa kwa *percentage* kiasi gani? Karibu 90 percent, siyo Tanzania peke yake. Kwa hiyo, huo mfumo unaoitwa *neutral*, siyo *neutral*, wala hautufai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, Mahakama zetu ni nzuri sasa hivi. Zimefanya maboresho makubwa mpaka tuna *Commercial Court* ambayo inasimamia masuala tu ya biashara na uwekezaji, Mahakama zetu zinaweza zikafanya kazi vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mpango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako tukufu kwa kunipatia nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala huu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*The Public Private Partnership (Amendment Act) Bill, (No. 5) 2018*). Nakushukuru kwa kuongoza mjadala wa muswada huu kwa umahiri na kwa msingi huo maoni na michango iliyotolewa imeiwezesha Serikali kuboresha maudhui ya muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuujadili muswada, maoni na ushauri waliotupatia Kamati baada ya kusikiliza maoni ya wadau, yametusaidia kuboresha maudhui ya muswada huu kama majedwali ya marekebisho yanavyosomeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Mheshimiwa Halima James Mdee kwa hotuba aliyoitoa kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia shughuli za Serikali vizuri kwa kutupatia ushauri na maelekezo kila siku ambayo yametuimarisha na kuboresha utendaji wetu wa kazi. Nawashukuru sana Mawaziri, Naibu

Mawaziri, Makatibu Wakuu kwa ushirikiano ambao walituonesha mimi pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa maandalizi na majadiliano ya muswada huu katika hatua zote. Pia nawashukuru watendaji wa Wizara walioshiriki kwenye hatua za maandalizi na majadiliano ya muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa muswada huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 37 wamechangia muswada huu, kwa hiyo kwa namna ya pekee ninawashukuru Wabunge wote waliochangia 31 kwa kuongea na sita kwa maandishi. Kipekee nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Adelardus Kilangi kwa ufanuzi mahiri wa maeneo ya kisheria yaliyogusa muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri waliyoitao wakati wa majadiliano kwenye Kamati na hapa ndani ya Bunge, bila kuwasahau Wabunge walioleta majedwali ya marekebisho. Tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha muswada huu na kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia muswada huu kwa kweli ni ushahidi kwamba Bunge hili linatambua umuhimu wa mapendekezo ya kurekebisha hii sheria na katika michango yao Wabunge wametoa hoja mbalimbali ambazo na mimi ningependa nizitolee ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilitoa hoja kwamba Serikali iweke sharti kwa Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa kumjulisha Waziri husika kuhusiana na orodha ya miradi ya ubia inayopendekezwa kabla ya kuwasilishwa kwenye kituo cha ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu wa Kamati wa kurekebisha kifungu cha 4(6) ili kuweka sharti ya kuzitaka Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali kumjulisha Waziri

husika kwenye Kituo cha Ubia (*PPP Center*) tumelizingatia na tumeongeza jedwali la nyongeza la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ya Bunge ya Bajeti iliishauri Serikali itumie mwongozo wa kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuhakikisha mabadiliko haya yanakuwa na tija, lakini pia kuwa Serikali iwezeshe Mfuko wa Uwezeshaji wa Miradi ya Ubia ili uweze kukidhi mahitaji ya msingi ya miradi. Serikali iweke mazingira wezeshi ili kuongeza Benki za Uwekezaji nchini kuongeza miradi ya ubia lakini pia Kituo cha Ubia kiwe na mpango mkakati wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma kwamba Serikali ifanye mabadiliko kwenye sera na sheria ya uwekezaji ili izingatie uwezeshaji kwenye miradi ya ubia na kwamba Serikali iimarishe soko la mitaji na hisa kwa kuangalia taratibu nyingine zitakazosaidia upatikanaji wa mitaji kupitia masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa kifupi kwamba Serikali imepokea ushauri huu mzuri wa Kamati na itauzingatia katika utekelezaji wa programu na mikakati ya kuimarishe utekelezaji wa *PPP* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani alishauri kwamba utendaji wa Serikali unaonesha kwamba tunarudi kwenye sera za ujamaa ambapo sekta binafsi hairuhuswi kujenga uchumi. Lakini pia alihoji ni nani msimamizi wa *PPP* pia akataka tafsiri ya neno Wizara, Waziri kwamba haijaeleweka bayana ni nani msimamizi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inaweka misingi ya uchumi imara kwa kuushirikisha sekta binafsi kuendesha uchumi nchini ambapo mipango ya maendeleo imekuwa inaweka bayana dhamira hii ya Serikali na ni dhahiri kuwa ukuaji wa uchumi wetu unachangiwa na sekta binafsi kama *engine* ya ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa ujumla. Hili linadhahirishwa kwa kutunga sheria, sera pia taasisi zinazoruhusu ushirikishwaji huu wa sekta binafsi. Mfano wa dhahiri kabisa ni nii sheria ya uwekezaji Tanzania, lakini pia sheria ambayo tunaifanya marekebisho sasa kati ya sekta

ya umma na sekta binafsi. Kwa hiyo, kwa kuzingatia ukweli huu Serikali imewasilisha mapendelekezo ya marekebisho ili kushirikisha sekta binafsi na kutoa fursa kwa sekta hiyo kutekeleza miradi ambayo inahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa mujibu wa kanuni na mgawanyo wa utekelezaji wa majukumu ya Mawaziri kama nilivyosema wakati ninawasilisha hoja, kanuni namba 144 ya mwaka 2016, imeweka bayana kwamba masuala ya *PPP* yanasi mamiwa na Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa tafsiri ya neno Waziri na Wizara, muswada unapendekeza tafsiri ya neno *Minister* na *Ministry* au Waziri na Wizara inayosimamia masuala ya *PPP* na kama Mwenyekiti aliyekuwa anaongoza kikao aliviyolieleza vizuri, tunataka kuondoa hitaji la kufanya marekebisho ya mara kwa mara hasa pale ambapo usimamizi wa *PPP* unakuwa umehamishiwa Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwepo mchango wa Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Omari Kigua na Dkt. Immaculate Sware Semesi. Kimsingi kulikuwa na mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na kwamba siku za kuidhinisha miradi chini ya kifungu cha 7(a) ni nyingi na wao walipendekeza zipunguzwe kutoka siku 21 hadi 10, lakini pia kwamba benki itakayotumika katika mradi wa *PPP* itegemeetie makubaliano kati ya Serikali na wabia badala ya kufungua akaunti hiyo Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa siku 21 umewekwa kwa kuzingatia ukubwa wa uchambuzi ambaa unatakiwa kufanyika kwenye mradi husika ili tuepuke hasara zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi hii tunategemea mingine iwe mikubwa na ya thamani kubwa sana, kwa hiyo hatutaki kuifanya kwa haraka haraka, tunataka tujiridhishe na tunaamini kwamba kwa kuangalia pia uzoefu wa nchi nyingine tunaona kwamba siku 21 zitatuwezesha kufanya hiyo kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa benki itakayotumika, kifungu cha 9 cha muswada hakibainishi sharti la kufungua akaunti ya mradi Benki Kuu, mapendekezo ya marekebisho yanakusudia kuondoa sharti la kufungua akaunti Benki Kuu na hivyo kufungua katika benki yoyote badala ya Benki Mahiri ya Uwekezaji. Pia akaunti inayozungumziwa hapa ni kwa ajili ya mfuko wa uwezeshaji yaani *PPP Facilitation Fund* na siyo akaunti kwa ajili ya wabia kuweka fedha zao za kutekeleza mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja kwamba miradi ambayo ni *unsolicited* isiwekewe masharti yoyote. Masharti ambayo tumependekeza lengo lake ni kuwa na miradi yenye tija kwa Taifa na hivyo kuepuka kuwa na miradi mibovu kwa kusingizia kuwa kiuhalisia na uzoefu tulipata tunataka kukwepa wawekezaji amba siyo makini, amba siyo wamekuwa wanawasilisha miradi Serikali ambayo hawakuwa wamepanga kuitekeleza na pia miradi mingine kutokuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano, kama hatutaweka masharti haya upo uwezekano kabisa wa kupata *unsolicited proposal* ambayo inaleta mradi amba unashindana na mradi mwengine amba Serikali imepanga kufanya. Pia upo uwezekano wa kupata miradi ambayo haina tija kwa Taifa letu, kwa hiyo, ni muhimu sana haya masharti yakawepo kwa *unsolicited proposal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia kwamba muda uliopendekezwa katika kifungu cha 12 cha miezi sita badala ya kila robo mwaka ni mrefu sana. Huu muda wa miezi sita (nusu mwaka) ni muafaka kwa kuwa Serikali huwa inawasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti yake kila nusu mwaka.

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka kwamba tulifanya marekebisho kwenye Sheria ya Bajeti ili tuwe na muda wa uhalisia ambapo Baraza la Mawaziri linafanya marejeo ya utekelezaji wa bajeti na hivyo utekelezaji wa miradi ya *PPP* pia itafuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mawazo kwamba *PPP* Centeriwe Idara ndani ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*T/C*) ili kupunguza gharama kwa Serikali. Miradi ya ubia ambayo inatekelezwa chini ya sheria hii ni tofauti na ile ambayo inatekelezwa chini ya Sheria ya Uwekezaji na Sura ya 38 ambayo ndiyo miradi ya kibashara kwa asilimia 100, kabla ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya mwaka 2014 kitengo cha uratibu wa *PPPKilikuwa* chini ya *T/C* ambapo utekelezaji wa uratibu wa miradi ya *PPP* ulioneckana kuwa na changamoto na hivyo kusababisha Serikali kufanya marekebisho ya sheria hii mwaka 2014, kwa hiyo bado tunapenda kulishauri Bunge lako tukufu kwamba hiki kituo kisiwe ndani ya *T/C*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Mollel alishauri kwamba utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ishirikishe sekta binafsi kupitia *PPP*. Sina ugomvi na hili lakini nilitaka tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, si zamani sana tarehe 2 Mei tulikuwa na ugeni wa watu maarufu Profesa Joseph Stiglitz ambaye mnajua ni mshindi wa Nobel ya uchumi lakini pia amewahi kuwa *Chief Economist* wa Benki ya Dunia. Tulikuwa pia na Profesa Kaushik Basu naye amewahi kuwa *Chief Economist* wa Benki ya Dunia lakini pia tulikuwa na Profesa maarufu sana kutoka Uingereza, Mama mahiri Profesa Sabina Alkire na siku ile tulikuwa tunajadiliana kuhusu *equitable growth and human development in a resource based economy* kwa hapa Tanzania. Moja ya vitu ambavyo vilitushtua akili zetu, wabobezi hawa ambao miaka yote wamekuwa wanasisitiza kwamba tuende kwenye soko, walisisitiza sana siku ile umuhimu wa kuwa makini na kutumia *The State Strategically* katika kuharakisha maendeleo ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya azimio la mkutano ule, naomba uniruhusu niseme kwa kiingereza inasema; "*The State has a key role to play in the economy, by addressing market failures directly, directly providing goods and services in some circumstance.*" Katika mazingira ya Tanzania mtakumbuka kipindi fulani hapa tulitoa *challenge* hapa kwamba jamani katika mazingira ya nchi yetu hawa ambao

tunasema wawekezaji wapo, wako wapi? Tulitoa fursa hapa ambaye analeta mwekezaji aje awekeze kujenga reli ya kutoka Mtwara kwenda Mbambabay na matawi yake kwenda Mchuchuma na Liganga, aje! Mpaka leo hiyo *offer imeshindikana*. Kwa hiyo, tusijidanganye kabisa. Miradi ambayo inaweza kuwa *commercial* lakini ni *of national strategic importance* msiweke Serikali pembeni. Hivi tutakaa tungoje, tukae na hii reli iliyojengwa mwaka 1905 mpaka Yesu Kristo ateremke? Haiwezekani! Kwa hiyo, ninawasihi sana hivi vitu vingine, akili za kuambiwa tuchanganye na za kwetu kwa manufaa ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wazo kwamba asilimia tatu ya kiasi cha fedha ya miradi ya *PPP* ambayo inapendekezwa kama *commitment fee* swali lilikuwa ni kwamba hiyo *deposit* itawekwa wapi. Kiutaratibu fedha za aina hii zinahifadhiwa na *Accounting Officer*, Afisa Masuuli katika Akaunti za Amana (*Deposit Account*). Hata hivyo, kwa kuzingatia hoja hii, Serikali imeboresha kifungu cha 10(3)(a) katika jedwali la marekebisho kwa kumpa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni zitakazobainisha utaratibu wa utunzaji na urejeshaji wa hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilisemwa kwamba *commitment* ile ya asilimia tatu iondolewe katika miradi ya *unsolicited*. Dhamana ya kiwango kisichozidi asilimia tatu lengo letu ni kuhakikisha uwepo na uthibitisho na uhakika na nia ya mwekezaji katika kuwekeza kwenye miradi alioibuni. Utaratibu huu unatuwezesha kuepuka uwekezaji usiokuwa makini. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba hii asilimia tatu ibaki isiondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea mawazo mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein na Mheshimiwa Oran Njeza, hususan kuhusu kuwajengea uwezo wataalam wa sheria katika kufanya majadiliano ya mikataba na uandishi wa mikataba. Kwa kweli, huu ni ushauri mzuri na tutauzingatia. Kifungu cha 4(6) cha Sheria ya *PPP* kimebainisha maeneo ya fursa ambayo mwekezaji anaweza kuomba uwekezaji wa

PPP, lakini baada ya uchambuzi wa miradi kufanyika na kupata idhini ya Kamati ya Kuidhinisha Miradi (*Steering Committee*), miradi iliyoidhinishwa itatangazwa katika Gazeti la Serikali na magazeti mengine. Kwa hiyo, kabla ya hatua hizo ni vigumu kubainisha ni miradi ipi itatekelezwa kwa *PPP* ili itangazwe kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki namshukuru sana kwa darasa lake zuri sana kuhusu *PPP*. Kwa kweli alitoa elimu nzuri na tunapokea ushauri kama Serikali na tutauzingatia wakati wa kuingia mikataba na kutoa hakikisho kulingana na mahitaji ambayo yanahusika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauriwa na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein kwamba Serikali itenye bajeti ya miradi ya *PPP*. Tunapokea ushauri na tutauzingatia. Kupitia muswada huu imependekewza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti ili kuwezesha miradi ya *PPP* kutengewa bajeti. Mheshimiwa Mbaraka Dau alishauri kuwa na mawasiliano ndani ya Serikali kuhusu miradi ya Serikali inayotarajiwa kutekelezwa kwa *PPP* ili kuwa na kauli moja ndani ya Serikali. Huu ni ushauri mzuri na kwa kweli, inatakiwa iwe hivyo wakati wote. Kwa hiyo, tutaufanya kazi ili kuboresha mawasiliano ya kiutendaji ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Martha Umbula alishauri Serikali itekeleze andiko la kimkakati (*blueprint*) ili kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwemo miradi ya *PPP*. Ushauri ni mzuri na tutaufanya kazi ipasavyo. Kama ambavyo tumekuwa tunaeleza Baraza la Mawaziri lilishaujadili na lilishatoa maelekezo ili kuanza kuendelea kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala alishauri kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali awe Mjumbe kwenye Kamati ya Uidhinishwaji wa Miradi ya *PPP* ili kuondoa ulazima wa mikataba ya miradi ya *PPP* kupelekwa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya *vetting*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilifahamishe Bunge lako tukufu kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Mjumbe wa Kamati ya Maamuzi ya *PPP* yaani ile *Steering Committee*, lakini hata hivyo utaratibu wa kuwasilisha mkataba Ofisi ya *Attorney General* kwa ajili ya uhakiki, hili ni hitaji la kisheria chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (*The Attorney Generals' Discharge of Duties Functions Act, 2015*). Kwa hiyo, maana yake tu ni hiyo, bado miradi hii itabidi iende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali *for vetting*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishalisemea lile ushauri wa Mheshimiwa Njeza kwamba vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu wapewe mafunzo kuhusu *PPP*, tunaupokea kabisa ushauri huu ni ushauri mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chiza...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri muda wako umekwisha, nakuongezea, una bado una hoja nyingi? Basi malizia.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwa hiyo, nimalizie tu kwa kusema Mheshimiwa *Engineer Christopher Chiza* pia alitushauri kuhusu kutoa elimu juu ya uelewa wa *PPP* kwa watendaji ndani ya Serikali na sekta binafsi na juu ya miradi ya *unsolicited proposals*, ushauri tunaupokea na tutauzingatia. Na tumeweka vigezo kwa upande wa hiyo miradi ambayo ni *unsolicited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya naomba niahidi kwamba maelezo ya kina ya kufafanua hoja zote tulizozipokea tutayawasilisha kwenye meza yako kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono.
Tunaendelea Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Kati
ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 (*The
Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*)**

Ibara ya 1

(*Ibara lliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 2

Ibara ya 3

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 4

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti,
nimeleta marekebisho, lakini kulikuwa kuna makosa ya
kiuchapaji kwa hiyo, nitaomba nieleze *concept* halafu Waziri
anijiblu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yalikuwa kwenye clause 4(6) isomeke hivi; “*by inserting the words as stipulated in the National Development Plans after the words National Development Priorities.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hapa mapendekezo ya Serikali ambayo ameongeza kifungu kingine yalikuwa yanasoma kama ifuatavyo; “*provided that the potential Public Private Partnership projects complies with a National Development Priorities.*” Sasa mimi haya mabadiliko nikiyajumuisha itasoma kama ifuatavyo; “*Provided that the potential Public Private Partnership projects complies with the National Development Priorities as stipulated in the National Development Plans.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependekeza hili kwa sababu nchi yetu imekuwa ama inakuwa *guided* siku zote na mipango ya Taifa ambayo chama chochote kikiingia madarakani kinatakiwa kiende na hiyo *vision* pana ya Taifa. Sasa haya mabadiliko ya Waziri yakiachwa kama ilivyo inakuwa haina *instrument* ambayo ina-link zile *priorities* za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu ni madogo tu, ni ku-link hizo *priorities* ambazo Waziri anazisema, lakini ziendane sambamba na Mpango wa Taifa ambao *basically* huwa anausimamia yeye na Mpango wa Taifa umeeleza kwa kina tu mambo mengi ambayo ni kipaumbele cha Taifa, lakini sasa uanzaji wa utekelezaji ya nini kifanyike inategemea na zile *priorities* ambazo zimekuwa provided within.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu yalikuwa yanapendekeza hivyo.

MWENYEKITI: Serikali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Halima Mdee, lakini Serikali tunaomba ibaki kama ilivyo kwa sababu

ifuatayo; *Development Priorities* za Taifa lolote lile huwa ziko ndani ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa hilo. Kwa hiyo, unapotaja *development priorities* tayari umeshaigusa mipango ya maendeleo ya Taifa husika. Kwa hiyo, ndicho kuirudia tena kuongezea na *development plans*, kama anavyosema itakuwa ni marudio. Kwa hiyo, mimi namshawishi Mheshimiwa Halima akubaliane na mapendeleko ya Serikali kwa sababu *priorities* zetu ziko kwenye mipango yetu ya maendeleo.

SERIKALI: Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba wachangiaji waniunge mkono ama wachangie hii hoja. Nimesikiliza majibu ya Waziri, labda niseme hivi, hoja hapa ni hivi, kuna shida ambayo imekuwa ikijitokeza ambapo anapokuja kiongozi ama anaweza akaja kiongozi yejote akabadilishabadilisha vipaumbele, hiyo ndiyo hoja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza juzi hapa kwa mfano, kuhamia Dodoma. Ukiangalia ule mpango wa miaka mitano haimo, lakini amekuja Mheshimiwa Dkt. Magufuli amependezeshwa na kwa kadri anavyoona inafaa akadumbukiza, lakini ukiangalia ule Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano haimo, wala mwaka mmoja haimo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima umeshaelewka, umetoa hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, haimo. Kwa hiyo, hoja yangu hapa ni *simple kwamba tunakubaliana kimantiki kwamba kuna vipaumbele vya Taifa, tunakubaliana kimantiki, lakini lazima turejee ile instrument.*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, nimeshakuelewa. Hoja yako nimeshakuelewa na Serikali wamekujibu, enhee?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wajumbe ama Wabunge wenzangu wachangie hii hoja labda kitaelewka.

MWENYEKITI: Toa hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtola.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Wakati mwingine tunavutana kwa vitu ambavyo viko *very clear*, kinachotuongoza kama Taifa ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa na siyo vipaumbele vya Taifa. Vipaumbele vinachaguliwa kutoka kwenye mpango. Kwa hiyo, tunachotakiwa kukitunza, kikitaja kama *instrument*, ambacho mtu yejote akiingia madarakani atakifuata ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndani ya mpango ndiyo mtaweka vipaumbele vyenu, uanze na cha mwisho, uanze na cha tatu, uanze na cha nne, hiyo ndio inakuwa *matter of choice* ya waliokuwa madarakani wakati huo. Sasa hatuwezi tukauacha mpango eti tutangulize vipaumbele, vipaumbele vya Taifa vitoke kwenye mpango na ndiyo hoja ya Mheshimiwa Halima hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri wakati anasema hapa, nilifikiri Serikali itachukua kama *typing error* wakati wanaandika, lakini nalo linakuwa jambo la kujadiliana. Sioni kama tuna haja ya kuvutana katika hili.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Takwa la Mpango wa Taifa ni la Kikatiba, tunapoanza Bunge tunakuja wote kwa pamoja hapa baada ya kumaliza chaguzi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha

anatushirikisha wote hapa, tunachambua kwa pamoja kama Wabunge, tunaandika na tunatungia sheria kuutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Halima Mdee anachokisema pamoja na mawazo mazuri hayo ya Serikali, Mheshimiwa Halima anasema, lakini *i-bind* kabisa kwamba hivyo *vipaumbele lazima vi-comply* na Mpango wa Taifa. Ni jambo dogo ambalo ni kuweka tu huo mstari ambao hamtapungukiwa chochote Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba ili yeyote anayekuwa isiwe kila siku tunaamka hapa mtu anaamua asubuhi mimi *priority* yangu ni hii, ni hii, alazimishwe yeyote atakapoingia madarakani kutekeleza Mpango wa Taifa, ajue kwamba anakuwa *bound* na Mpango wa Taifa alazimishwe yeyote atakayekuwa. Kwa hiyo, itakuwa ni *instrument* itakayotusaidia sote kwa pamoja. Ningeomba Mheshimiwa Waziri akubaliane na hilo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tatizo hapa ni lugha na tafsiri ya kimaudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mtizamo wa kawaida ukisema mpango kwa maana ya *National Plans*, ni mpango mkubwa sana, lakini *priorities* ziko *listed* kwenye huo mpango mkubwa. Mpango wa Maendeleo kwa maana ya *Development Plans* haitekelezwi na *PPP* peke yake, inatekelezwa kwa njia nyingi, *PPP* ni sehemu mojawapo ya kuetkeleza mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia *PPP* kama sehemu mojawapo lazima *i-relay* kwenye *priorities*, na *priorities* zinabadilika kulingana na mazingira. Leo unaweza ukawa na *priority* hii, kesho ikabadilika kutokana na *situation* ambayo haikutarajiwa pengine. Kwa hiyo, *priority* inaweza ikabadilika, mpango ni mpaka tena urudi upitishwe. Kwa hiyo,

kwa sababu shughuli ya *PPP* ni ya Waziri, ya kila siku yaani akiamka hivi zimekuja-zimekuja, lazima a-deal na *priorities*, ikiwa ni mpango itabidi tuje tubadilishe hapa mpango, sijui tumelewana jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini mmenielewa. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Dkt. Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kunipa nafasi. Kwa maoni yangu mimi mpango wa maendeleo wa miaka mitano siyo sawa na kipaumbele, hauwezi kuwa sawa na kipaumbele, vilevile vipaumbele vinabadili kila wakati. Hata kwenye hii *clause* hapa au kwenye *sub section* hii hawajasema tusizingatia mpango wa maendeleo, *there is nothing like that* kwamba tusizingatia mpango wa maendeleo, ila wamesema kwamba *PPP* iende kwa *development priorities*. Nafikiri hii ni muhimu sana. Kama hatutakwenda kwa vipaumbele watu watakuja kufanya mambo yao wanayoyataka kwa mipango yao na syo kwa vipaumbele vyetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Serikali.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hii ibaki kama ilivyo kwenye muswada wenywewe. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Serikali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge, mimi naomba sana ibaki kama ilivyo kwa sababu kuna sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopata tetemeko Kagera, shule yangu ya Ihungo ikaanguka haikuwa kwenye mpango, lakini ilikuwa ni lazima twende tukajenge ile shule, vivyo hivyo, nchi nyingine madaraja yamebomoka

unafanyaje? Subirini, ndiyo maana bado ibaki *priorities*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu hivyo, Dodoma, jamani mapato ya nchi hii asilimia 85 yanatoka Dar es Salaam. Tulishakubaliana tutengeneze *growth poles* nydingine za nchi na Dodoma ni mojawapo. Sasa Dodoma inagomba kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge tuishie hapo ibakie *priorities* za Taifa. Hakuna mahali, kama Mheshimiwa Dkt. Nagu anavyosema ambapo tuna-*ignore Mpango* wa Maendeleo wa Taifa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima funga hoja yako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu kama haya ndiyo yananifanya niseme ndiyo maana nchi yetu tuko hapa. Kumbe kama nchi hatuna *vision*, wala hatuna *mission*. Niulize swali jepesi, hivi kati ya mpango na kipaumbele kipi kinaanza? Kinaanza kipaumbele au unaanza mpango?

WABUNGE FULANI: Mpango.

MHE. HALIMA J. MDEE: *Seriously?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima unaweka mpango ndani ya mpango ndiyo kuna vipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikijibu hoja ambazo sijui zimetoka wapi, kwa mfano, kwani *spirit* ya kuanzisha, kuna hoja ya Mheshimiwa Simbachawene amesema sijui *National Development Plan* sijui na *PPP* ni vitu viwili tofauti. Mnatuambia kwamba mmeanzisha *PPP* kwa sababu mmejua Serikali hamuwezi kugharamia huduma kwa wananchi ndani ya muda kwa hiyo, mnahitaji msaada. Kwa hiyo, ndani ya ule mpango mpana kuna *deficity*. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima funga hoja yako. Umeshaelewaka, funga hoja yako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja kwamba dhamira ya kuomba nyongeza, wala siyo kubadilisha fikra za Serikali, kuomba nyongeza kwa ajili ya kusaidia Taifa tuwe na *continuation* ya mipango yetu ili tuweze kuitekeleza kwa ufanisi, bila kuwa na *continuation* ndiyo maana leo utasema kilimo kipaumbele... kesho unakuja unasema kipaumbele...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima unaanza mjadala, katika hatua hii sasa tulipofika hapa kama unaendelea na hoja yako omba tuingie katika maamuzi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Bunge liamue, kama twende bila *vision* ama twende na *mission* na *vision* ili tuweze kulisaidia Taifa hili. Naomba kura zipigwe. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)
(*Hoja lliamuliwa na Kukataliwa*)

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali*)

Ibara ya 5

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali*)

Ibara ya 6

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali*)

Ibara ya 9

MHE. ALLAN J. KIULA: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mdee; Mheshimiwa hebu kaa chini kwanza siyo kipindi cha utaratibu hiki. Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Waziri ambayo amesema kwamba fedha za wawekezaji...

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida kidogo kwa sababu karatasi niliyonayo mimi chini imesema *dated* tarehe 12 Novemba, 2018. Sasa hii karatasi tunajadili mbona imekuja kabla ya muda? (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa kuna muhuri wa Bunge wa Septemba. Tunaendelea na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ndio maana hata mwanzo nilisema kwamba kuna maeneo yana makosa ya uchapaji. Kwa majibu ya Waziri ambayo amesema fedha hizi za wabia hazitawekwa *BOT* na kwamba zitawekwa kwenye benki ya kawaida watakayokubaliana, ninatoa haya marekebisho.

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 10

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo muswada umeonesha kwamba kuna takwa la kuweka asilimia tatu ya fedha kama *commitment*. Sasa ukija kwenye kifungu hiki, kifungu kidogo cha (e) kinasema; “*The Minister may make regulations prescribing procedure for refund of committed deposit under sub section 3.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajua kwamba tunapotunga sheria huwa kuna vifungu ambavyo vinampa mamlaka Waziri kutengeneza *regulations*. Anaweza akatengeneza ama asitengeneze kutohana na mahitaji na sheria jinsi ambavyo imejisheheni. Sasa kifungu hiki *specific*, ndiyo maana sijaomba mabadiliko kwenye maeneo mengine ambayo yanamtaka Waziri atengeneze *regulations*, kifungu hiki *specific* Mheshimiwa Waziri anachukua fedha za watu lakini wakati huo huo sheria inamwambia anaweza akaweka mlongozo, sasa haimlazimishi kuweka mlongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaweza tukajikuta pesa imechukuliwa mwongozo haujawekwa *in place* halafu mtu anataka kuchukua chake kwa sababu yale makubaliano yameshindwa, wameshindwana, inakuwa taabu. Kwa hiyo lengo hapa ni kumtaka Waziri kwa kuwa amekubali kwamba *that three percent* inachukuliwa, basi alazimike kutengeneza *regulations specifically* kwa utaratibu wa urejeshwaji wa hizo fedha. Kitu kidogo tu.

MWENYEKITI: Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza na kumwelewa vizuri sana Mheshimiwa Halima, lakini yeye ni Mwanasheria na anajua kwamba zipo *principles* za uandishi wa sheria. Katika masuala yote yanayohusu kumwelekeza Mheshimiwa Waziri kutengeneza *regulations* siku zote neno linalotumika ni *may* na *shall*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba ni kweli kwamba miongozo inayotumika kisheria kumtaka Waziri atengeneze *regulations* inasemekana *may* kwa mantikl ya kwamba anaweza kwa kutambua hivi. Kuna mazingira mengine sheria haihitaji kutengeneza *regulations*, kuna mazingira mengine sheria inalazimika kutengeneza *regulations* ili kulazimisha sasa ama kuwezesha utekeleza wa sheria kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nimesema hivi kuna maeneo mengine kwenye hii sheria yameeleza kwamba Waziri anaweza akatengeza *regulations* sijahangaika nayo kwa sababu yeye ataangalia namna gani sheria itamwezesha kufanya kazi au haimwezeshi. Lakini kwa hiki kifungu mahsus ambacho kuna cha watu kimechukuliwa na halazimiki kutengeneza, anaweza akatengeneza kwa utashi wake yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani hiyo *commitment* ni muhimu na nitaomba kifungu hiki kijadiliwe kama sitapata majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Mmechelewa kusimama.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Ndio ukweli wenyewe mmechelewa. Waheshimiwa tuko Bungeni humu ndani. Mheshimiwa Halima umesema umekaa, aliyesimama ni Dkt. Sware na Mheshimiwa Hawa, wengine wote mmekaa.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 11

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja nimeomba yafanyike marekebisho kwa mantiki ya kwamba ukifute hiki kifungu kilichokuwepo, lakini vilevile kurudisha kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkoo wa Serikali amejaribu kueleza kujibu hoja ambayo tumesema kwamba *dispute* yoyote ambayo *it-a-rise during the course of the agreement shall be resolved through negotiation, mediation na arbitration.* Kifungu hiki kilikuwepo kwenye sheria ya PPP ya zamani ambayo inarekebishwa sasa, hiyo mosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumesema hivi, unapomtaka mwekezaji aje na hakuna popote katika mabadiliko yangu ambayo Mwanasheria Mkoo wa Serikali amejibu, niliposema kwamba hatutaki taratibu za ndani zisitumike hakuna popote niliposema. Nilichosema ni kwamba katika uhalisia wa kawaida na kwa vifungu ambavyo tumeviongeza ambavyo vinaweka masharti makali kwenye *unsolicited projects* ni muhimu mtu anayeleta pesa zake kwa asilimia 100 a-*feel comfortable* katika mkataba kukubaliana mtaweza ku-*resolve dispute* zenu katika mazingira gani. Mnaweza mkakubaliana mazingira ya ndani mnaweza mkakubaliana mazingira ya nje kwa kadri ambavyo mkataba kati ya Serikali na huyo mwekezaji watakavyoingia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimeshangaa sana Mwanasheria Mkoo wa Serikali anatoa mifano ya Iran. Hivi utalinganisha uchumi wa Tanzania na wa Iran? Sasa tuache kujidanganya na kujifungia ndani ya *box*. Labda atuambie, hii PPP ambayo tunairekebisha ambayo mimi nimerudisha kifungu kama kilivyokuwa mwanzo... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, hebu kaa kwanza. Mheshimiwa *Chief Whip.*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ninaomba kutoa hoja

Bunge hili na katika hoja ambayo imewekwa mezani leo asubuhi basi kikao chako kiendelee mpaka tutakapokuwa tumeikamisha hoja hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja Iilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu naomba ni-summarize kama ifuatavyo:-

Kwamba *PPP* tunayoipitisha leo ina sura mbili, ita-*attract* wawekezaji wa ndani, ita-*attract* wawekezaji wa nje. Ina sura mbili, kuna *project* ambazo Serikali inaweza ika-*fund* kwa kushirikiana na watu binafsi, kuna *project* ambazo watu binafsi wa ndani na wa nje wata-*fund* wenye. Sasa kwa kuzingatia hivyo ni muhimu tuwe halisi, kwa mantiki ya kwamba siwezi mimi Halima nimetoka labda Marekani ama ninatoka Japan unakuja kunilazimisha kwamba lazima mfumo wa kimahakama wa ndani ndio uweze ku-*settle dispute* wakati tunajua kwamba kuna mazingira ambayo mifumo yetu ya kimahakama ya ndani haijaka sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba mabadiliko haya yaliyopendekezwa na Serikali yaondolewe ili kutoa *avenue* kuweza kutatua ndani ama kutatua nje kwa kadri ambayo mwekezaji ataona na Serikali itaona inafaa kutokana na mahitaji na *complication* za mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo asiponijibu nitakuja kutoa hoja ili Wabunge wachangie.

MWENYEKITI: Ahsante, Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Halima anasema hakusema mahali popote kwamba haungi mkono utumiaji wa mahakama za ndani. Naomba nirejee kwenye hotuba aliyoisoma jana ukurasa wa 9 *paragraph* ya mwisho;

"Mheshimiwa Spika, mbali na ukweli kwamba tunazipenda na kuziheshimu sana mahakama zetu ni ukweli vilevile kwamba *PPP*inahusisha wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje. Mwekezaji yeote makini anataka kwenda katika mahakama za usuluhishi wa masuala ya kibiashara ambazo ziko *neutral*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa anacheza na *logic*, ukishasema huhitaji mahakama za ndani, unabakiza mahakama zipi? Ni mahakama za nje, kwa hiyo, hata ukisema mahakama *neutral* unazotaka umeshasema za ndani hauziamini maana yake by *necessary implication* unasema unataka mahakama za nje. Kwa hiyo, katika hilo naomba liwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye mapendekezo anayotoa Mheshimiwa Halima; anasema tuweke kifungu kwamba *any dispute arising during the cause of agreement shall be resolved though negation, mediation or arbitration*. Ameiacha hivyo wazi bila kuonesha ni mahakama za ndani au za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *formulation* ya Mheshimiwa Halima ina mtego, ni mtego ambao ninauona kwenye *bilateral investment treaties* nydingi kwenye *investors state agreement* nydingi. Mtego unaowekwa wanafanya kama wameiacha hivi iko *neutral* lakini baadae *tribunal* zitatafsiri kwamba hii *mediation or arbitration* inayozungumzwa inaweza ikafanyika ndani ya nchi au nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali msimamo wake ni kwamba haya yote yafanyike ndani ya nchi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali amalizie sentensi. Nirudie; nimesema hivi utaratibu huu wa kutumia...

"Mheshimiwa Spika, mbali na ukweli kwamba tunazipenda na kuziheshimu sana mahakama zetu ni kweli vilevile kwamba PPPitahusisha wawekezaji wa ndani na wa nje. Mwekezaji yejote makini anataka kwenda katika mahakama za usuluhishi na masuala ya kibiashara ambazo ziko *neutral*. Utaratibu huu wa kutumia mahakama za ndani pekee utawafukuza wawekezaji makini wa nje hasa kwa kuzingatia kwamba kuna miradi ambayo inatarajia wawekezaji kutumia pesa zao za ndani wenyewe kwa asilimia 100." Haya ndio maneno yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilisema hivi, sisi kama nchi si kisiwa, sisi kama nchi ni *signatories* wa mikataba mbalimbali ya kimataifa na ni *member* wa mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo kama nchi tumesaini na mikataba husika inahusiana na masuala ya uwekezaji. Sasa kama dhamira yetu ni kupata watu *serious, then* suala la *neutrality* ni la muhimu. Kama dhamira yetu ni kujifurahisha na kujidanganya kwa sababu kuna nchi kadhaa zimejifungia kwenye *box* na kuamini mna mifumo bora ya kimahakama inayotambulika na kuheshimika katika jumuiya za kimataifa *then* ni ninyi wakuamua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sasa niruhusu Wabunge wachangie, kwa sababu jana tu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima ushafikia hatua sasa ya kuchangia.

MHE. HALIMA J. MDEE: ...tumeeleza kiwango kipana sana na tunaomba Wabunge wachaingie hii hoja ili sasa tuamue kwa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Tushasimama sababu ushapigwa bao kwanza. Ahsante. Tunaanza na Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Unajua mara nyingi sana hata *incentives*

ambazo Serikali yetu ilikuwa ikitoa kwa wawekezaji ni katika hali ya kuvutia wawekeza kutokana na uchanga wetu na miundombinu hata tulionayo. Kuna wakati Serikali hii hii inawapatia watu *tax holiday*. Kwa mfano kwenye madini wanachimba hawalipi kodi kwa muda fulani ili kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira tuliyonayo ni yale yale. Leo huwezi kumwita mwekezaji kutoka nje kwenye mahakama ambazo zinafuata maelekezo ya wanasiasa kwa mfano, hakuna mtu atakuja hapo akaja kuwasikiliza kwa sababu kauli zetu wenyewe mara nyingi sana zimekuwa zikikinzana na utawala bora, na sisi hatuko kwenye kisiwa. Sasa mtu anakuja hapa anatuambia sijui Iran, sijui walifanya nini. Iran hawapambani na matundu ya choo. Leo sisi miaka 56 bodo tunahangaika kuchimba matundu ya choo. Tunahitaji fedha za kutosha katika ... (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha, Mheshimiwa Ally Saleh (Albeto).

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajidanganya kwamba hata tukiweka katika sheria yetu kwamba kesi hazitafika huko katika mahakama za kimataifa haitazuia kwenda kwenye mikataba ya kimataifa. Yule mtu anayekuja kuweka pesa zake hapa amekopa nchini kwake kwenye mabenki ambayo anawajibika kuchukua hatua, kwa hiyo hii inatoa-*option*. Sasa cha kufanya ni kwamba tujenge *confidence* kwa wawekezaji, tujenge *predictability* mtu aweze ku-*predict*; lakini pili kama tunataka kuzuia ni kama walivyosema wengine tujipange kama Taifa, tuwe na watengeneza mikataba wazuri tuwe tunatekeleza wajibu wetu ili tuepuke lakini *option* ya Halima *the best* ili kama kutaka kuvutia wawekezaji, la kama unataka kujidanganya... (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kakunda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA): Mheshimiwa

Mwenyekiti, inahitaji uzalendo kuweza kujadili vizuri sana hoja hii. Kwa sababu nchi hii ni nchi huru na mtu ye yote yule duniani kokote kule anayetaka kuja kuwekeza Tanzania kuitia mikataba ambayo huwa inaanza kwanza na mkataba wa makubaliano halafu baadae mnakuja kuingia mkataba wa kibiashara. Atakayekubali kusaini mkataba wa kibiashara kule ndani ya mkataba wa kibiashara kuna hiyo *clause* ambayo itamwambia masuala yote ya usuluhishi yatafanyika hapa Tanzania kuitia mahakama zetu, huo ndio uzalendo tunaoutaka. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika mahala penye jambo la kizalendo na hasa kwa kuwa Tanzania tumejipambanua kuitia sheria zetu tulizotunga mwaka jana...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Heche! tuko Bungeni Waheshimiwa. Mheshimiwa Simbachawene endelea.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika katika hatua hii ni lazima tuijulize hiyo *neutral ground* iko wapi katika usuluhishi wa migogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama hizo zinazotumika na kampuni hizo kubwa za kimataifa hao hao ndiyo wanao-*finance* mahakama hizo. Hata hivyo Tanzania kama nchi ambayo tuna *legal system*, nchi huru yenye *sovereignty* kati yetu sisi wenyewe tunadharau mfumo wa kwetu wa *dispute settlement* kuna mashaka makubwa ya uzalendo wa baadhi ya wenzenetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ushauri wangu ni kwamba mwaka jana tulitunga Sheria ya *Natural Wealthy* na *Unconscionable Terms*, tuliweka *provision* hii kwamba migogo yote ya uwekezaji itasuluhishwa hapa nchini.

Tunapotunga sheria hii hatuwezi tukawa na *double standard*, tumeshajipambanua hivyo kwa dunia... (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante umeshaelewaka. Serikali cha kuongezea.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya mikakati mikubwa kabisa inayotumia na wawekezaji huwa ni kuzitisha hasa nchi zinazoendelea na wanatisha kwa kusema mkifanya jambo hili mtaondoa *investor confidence*, hamtavutia wawekezaji, wawekezaji watakimbia na hawataki mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *survey* imeshafanyika nchi mbalimbali wawekezaji hawakimbii hata mabadiliko yanapofanyika lakini tumeshasema hakuna *neutral ground*, hivyo vyombo vyote vinavyosema vya kimatalfa *they are not neutral* nimeshaeleza kiasi cha kutosha. *On top of that* vina gharama kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hapa hatupendi sisi kujiona kwamba tunaweza kufanya kitu cha maana, tunajidharau. Tulivyopitisha zile sheria mbili mwaka jana zipo nchi nyingi sana si Afrika, nje ya Afrika zinazouliza na zimekuwa *so much inspired* mmefanyaje... (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante, subiri kwanza Halima.

Waheshimiwa mimi nafikiri hii ni hoja ya msingi ya Serikali na siku zote upande wa *opposition* mnaitahadharisha Serikali kuhusu mikataba na namna tunavyopigwa, cha ajabu kila tukishindwa kesi za kimataifa kwenye mitandao watu wanachekelea, watu wanafurahi kabisa tume pigwa.

Sasa *natural resources* za nchi siyo mapapai, haziozi na hazitaoza, *natural resources should be used for the benefit of the people* siyo *comfort* ya *investor*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia, kwa sababu labda hukuwepo nilisema hivi; tunashindwa kwenye kesi za kimataifa siyo kwa sababu nydingine, mosi, kwa sababu kama nchi miaka yote tumekuwa kupitia watu ambao tumewaamini kwa nafasi mbalimbali za kuingia mikataba wakiingia mikataba mibovu ambayo haiangalii maslahi ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jana nilisema hivi shida yetu ya msingi; unakumbuka ACACIA na makinikia hapa; tutarudi hapa. Shida yetu ya msingi siyo mahakama, shida za msingi ni sisi ya kwanza na mikataba. La pili, sisi hatuwacheki ila sisi tunawakebehi kwa sababu tulishauri mkatupuuza... (*Makof*)

MWENYEKITI: Haya tumefika hatua ya kuhoji, Mheshimiwa Halima hatupo katika michango, tupo katika kuhoji.

MHE. HALIMA J. MDEE: (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: *No! no! no!* Halima tupo katika hatua ya kuhoji sasa kama umeridhika na Serikali sema twende mbele, hujaridhika toa hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu, namshangaa sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwanza mnajifanya *sovereign state*, pili mnajifanya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima hapana! Serikali imesha-*stand firm*, sasa inabaki hatua yako ya kikanuni, huna haja ya kujibu hoja, tunabaki kuhoji Bunge sasa hivi. Kama umekubaliana na Serikali tunaendelea la hukubaliani na Serikali kanuni zinakupa fursa tuingie katika kunini, ndiyo hiyo sasa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi sikubaliani na Serikali kwa sababu hoja zake ni mfu na haziendani na hali halisi.

MWENYEKITI: Toa hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MBUNGE FULANI: Ameshatoa hoja

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. HALIMA J. MDEE: Tupige kura jamani, mbona mna mapepe? Tulieni! Naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Haya, ahsante

MBUNGE FULANI: Ni kura.

MHE. HALIMA J. MDEE: Tupige kura.

*(Hoja llitolewa lamuliwe)
(Hoja lliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba
Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae, Mtoa Hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa
Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge
Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
ya Ubina Bainaha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*The Public
Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*) kifungu kwa
kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja
kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makof)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika wakati wa utekelezaji wa sheria hiyo (*A Bill for an Act to amend the Public Private Partnership Act in order to keep the law updated with challenges observed in its implementation*).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwa hatua ya Bunge tumemalliza kazi, hongera sana Mheshimiwa Waziri, *Attorney General*, Manaibu, Wabunge, na hongera Mheshiniwa Halima Mdee kwa hoja zako na kila hoja ambayo umeleta imejibowi vizuri. Nawapongeza Wabunge wote kwa michango yenu, sasa sheria inakwenda kwenye hatua ya Mheshimiwa Rais kuipitisha na kuiidhinisha.

Baada ya maneno haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.09 mchana Bunge liliahriishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 13 Septemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*